Mwamshe Mlinzi

Kuanzisha lindo za maombi za 24-7

Kiswahili

SEHEMU YA 1:

Msimulizi na viielelezo vya maombi iya usiku na mchana
Kuanzisha lindo za maombi za 24-7
Msimulizi na vielelezo vya maombi ya usiku na mchana
1:1 Agano la Kale
1:2 Waesene
1:3 Kanisa la kwanza la Kikristo
1:4 Jangwa la Misri
1:5 Wamoraviani
1:6 Nyumba ya Kimataifa ya Maombi (NYKYM – Jiji la Kansas)
1;7 Nyumba ya Yerusalemu ya Maombi kwa Mataifa yote
1:8 Poland 24
1:9 Lindo la Maombi Marekani/DC, Washington DC, Marekani
1:10 Minara ya Maombi huko Indonesia
1:11 Lindo za Maombi kwa watawaliwa wa madawa ya kulevya
1:12 Vyumba vya maombi katika makanisa
1:13 Miji kumi na tano katika mzunguko wa maombi wa majuma 5
1:14 Kitongoji/kambi ya wavamiaji ikikolzwa kwa lindo za maombi
1:15 Vijana na 24/7
1:16 Medhehebu na mashirika ya Kikristo
1:17 Milima ya Maombi
1:18 Lindo za maombi za Neno
1:19 Magereza

Sehemu ya 2:

Sababu ya maombi ya usiku na mchana
2:1 Msingi wa Maandiko kwa ajili ya maombi ya mchana-na-usiku
2:2 Faida ya maombi ya mchana-na-usiku
2:3 Maombi na utendaji
2:4 Uchunguzi mfupi juu ya matumizi ya neno "lindo" katika Maandiko

Sehemu ya 3:

Miongozo ya jumla
3:1 Mahali pa kukutania panapotumiwa kwa ajili ya lindo za maombi
3:2 Mitazamo mbalimbali ya kuwafanya watu wahusike
3:3 Marudio ya kuhusika
3:4 Majina mbalimbali yanatumiwa kwa lindo za maombi za mchana-na-usiku
3:5 Lengo la maombi ya lindo za maombi
3:6 Tovuti za kusaidia

Sehemu ya 4:

Jinsi ya kuendesha chumba cha maombi
4:1 Miongozo ya lindo za maombi za 24-7-365
4:2 Thamani na kanuni kwa ajili ya kujenga lindo za maombi za 24/7/365
4:3 Miongozo kwa ajili ya kuanzisha lindo za maombi za 24/7 (saa 168)
1. Kanuni za msingi za kukumbuka wakati wa kuanzisha lindo za maombi
2. Miongozo ya ujumla
3. Jinsi ya kuendesha chumba cha maombi cha 24-7
4. Mawazo mengine machache

4:4 Mfano wa chumba cha maombi cha kuingiliana pamoja na vituo vya maombi

Sehemu ya 5:

Nini cha kuombea
5:1 Baadhi ya miongozo ya jumla juu ya nini cha kuombea
5:2 Viashiria vya maombi vya kutumia ili kuombea jumuiya, mji/jiji, nchi na ulimwengu wako.

Sehemu ya 6:

Jinsi ya kutumia saa moja katika maombi: Muhtasari wa Maombi ya saa moja.
6:1 Kielelezo 1: Tafuta Uso Wangu
6:2 Kielelezo 2: Saa inayoubadilisha ulimwengu

Sehemu ya 7:
Kuomba Neno
7:1 Kwa nini tunapaswa kuomba Neno
7:2 Jinsi ya kuomba Neno
7:3 Maombi 30 ya Neno

Nimeweka walinzi juu ya kuta zako, Ee Yerusalemu; hawatanyamaza mchana wala usiku … na kwa maombi yenu Bwana azikumbuke ahadi zake … na msimwacha akae kimya hadi … Isa 62: 6 – 7.

Kuna tofauti kubwa sana kati ya kusema maombi na kuomba – John G. Lake.

SEHEMU YA 1.
Msimulizi na viielelezo vya maombi iya usiku na mchana
Kuanzisha lindo za maombi za 24-7
Msimulizi na vielelezo vya maombi ya usiku-na-mchana

1:1 Agano la Kale
1:2 Waesene
1:3 Kanisa la kwanza la Kikristo
1:4 Jangwa la Misri
1:5 Wamoraviani
1:6 Nyumba ya Kimataifa ya Maombi (NYKYM – Jiji la Kansas)
1;7 Nyumba ya Yerusalemu ya Maombi kwa Mataifa yote
1:8 Poland 24
1:9 Lindo la Maombi Marekani/DC, Washington DC, Marekani
1:10 Minara ya Maombi katika Indonesia
1:11 Lindo za Maombi kwa watawaliwa wa madawa ya kulevya
1:12 Vyumba vya maombi katika makanisa
1:13 Miji kumii na tano katika mzunguko wa maombi wa majuma 5
1:14 Kitongoji/kambi ya wavamiaji ikikolezwa kwa lindo za maombi
1:15 Vijana na 24/7
1:16 Medhehebu na mashirika ya Kikristo
1:17 Milima ya Maombi
1:18 Lindo za maombi za Neno
1:19 Magereza

Masimulizi na vielelezo vya lindo za maombi za 24-7

Tangu mwanzo wa 1990, kumekuwa na msisitizo mpya juu ya lindo za maombi za saa 24 duniani kote. Wendo huu, uliovuviwa na Mungu, unaenea katika ulimwengu wote. Kufikia katikati ya muongo uliotangulia, kulikuwa na dazeni chache tu za lindo za maombi za saa 24 zinazofanya kazi. Katika muda chini ya miaka kumi, idadi hii ilikuwa hadi maelfu machache. Lengo la lindo hizi za saa 24 ni kuwaweka walinzi juu ya kuta: ili kuhamasisha makanisa, mikoa na mataifa kumwendea Mungu katika sifa, kuabudu na maombezi, usiku-na-mchana.

Wendo wa maombi wa duniani kote unatekeleza mchakato mahususi wakati wa kuanzisha lindo za maombi.

Makanisa, miji, majiji, nchi na mabara yanahamasishwa kusimama mbele ya kiti cha enzi cha Mungu saa 24 kwa siku ili kumsifu na kumwabudu yeye na kuombea mataifa. Waombezi wanaombea uamsho katika kanisa na kwa ajili ya uinjilisti wa ulimwengu pamoja na mageuzi na uponyaji wa majiji na nchi. Kwa njia hii Amri Kuu na Agizo Kuu litatekelezwa.

Lililo bora ni kuyaitisha maelfu ya makanisa ili kuanzisha lindo za saa 24 katika jumuiya. Mahali pa kuanzia ni kupata sharika moja moja kuanza kuomba kwa saa 24 angalau mara moja kwa juma, na kisha kuongeza kipindi hiki hatua kwa hatua. Pili, makanisa yanatiwa moyo kuanzisha lindo la maombi la 24-7-365 pamoja na makanisa mengine ili kuombea jumuiya, mji/jiji na nchi yao kiuhalisi

kwa saa 24 kwa siku. Ndoto ni kuanzisha dhana hii katika kila nchi duniani. Lengo ni kuanzisha lindo za maombi katika kila mji, jiji na bara duniani ili kwamba mtiririko thabiti wa maombi kwa ajili ya dunia iliyovunjika na kuanguka yaletwe mbele ya kiti cha enzi cha Mungu.

Masimulizi na vielelezo vya lindo za maombi za 24-7

Aya zifuatazo zinadokeza mifano michache ya maombi ya usiku-na-mchana katika historia ya kanisa.

1:1 **Agano la Kale:** Katika Kutoka na Mambo ya Walawi tunasoma kwamba makuhani ilibidi waache taa zikiwaka katika hekalu. Bwana alikuwa mwenye kutiisha juu ya amri kwamba moto ule juu ya madhabahu kamwe usiruhusiwe kuzimika. Makuhani walifanya kazi kwa zamu ili kwamba hekalu lijazwe kwa maombi, kuabudu na wimbo kwa saa 24 kwa siku.

1:2 **Waesene:** Wakati ule wa Yesu moja ya matawi manne ya dini ya Kiyahudi, Waesene, waliamini katika kuomba kwa saa 24. Jumuiya iligawanywa mara tatu ili kwamba washike zamu kila siku ya tatu kukesha na kuomba usiku kucha.

1:3 **Kanisa la Kwanza la Kikristo:** Kanisa la kwanza lilizaliwa kutokana na maombi ya 24-7. Kwa ujumla inakubalika kwamba wanafunzi waliomba kwa pamoja na kwa siku kumi kabla Roho hajawashukia wakati wa Pentekoste.

1:4 **Jangwa la Misri:** Katika karne ya tatu na ya nne, Wakristo wengi huko Misri walikwenda jangwani ili kuomba na kutafakari. Wanaume na wanawake wengi wenye kumcha Mungu walifanya makazi jangwani. Leo hii kazi za baadhi ya watu hawa bado ni milingoti ya nuru. Kipindi hiki mara nyingi kinahusishwa kama wakati wa mababa wa jangwani. Ufuatao ni mfano wa wendo kama huo wa maombi. Katika sehemu ya magharibi ya jangwa la Misri, katika eneo linalojulikana kama Wadi El Natrun (Banda la Chumvi) Mt. Makarios alijenga nyumba nne za utawa. (Hizi hazikuwa nyumba pekee za utawa zilizojengwa katika eneo lile, bali zinakuwa kama mfano). Kati ya watawa wa kiume 8,000 na 10,000 waliishi katika upweke kwenye ujirani wa hizi nyumba za utawa (takriban 40,000 kwa jumla). Maombi ndiyo yalikuwa kazi yao muhimu sana. Waliomba kwa saa 12 hadi 20 kwa siku. Kila siku, waliomba hatua kwa hatua kupitia zile Zaburi 150, Manabii na sehemu kubwa ya Agano Jipya! Maombi haya, ambayo yalifanyika mchana-na-usiku, yaliongoza kwenye uamsho ulioenea kama moto toka Misri hadi Urusi. Injili ilienea kotekote katika Afrika yote ya Kaskazini. Kwa kweli watawa wa kiume, walikuwa na shughuli nyingi za

maombi ya saa 24. Waliomba Neno na ahadi za Mungu usiku-na-mchana. Waumini wanaweza kujifunza mengi kutoka kwa mtindo wa maisha ya maombi ya wale mababa wa jangwani. Mengi ya yanayotokea leo katika uga wa wendo wa maombi, ni maombi ya shirika/pamoja. Katika kanuni hii kuna nguvu, lakini pia udhaifu kwa sababu si lazima ikuze maisha binafsi ya maombi ya muumini.

1:5 **Wamoraviani:** Katika mwaka wa 1727, Wamoraviani huko Hermhut walianza lindo la maombi ya 24-7-365 yaliyodumishwa kwa miaka 125. Lilianza na wanaume na wanawake 48 ambao waliomba wawili wawili kwa saa moja moja. Baadaye waumini zaidi waliungana nao, pia vijana na watoto. Ndani ya miaka 25 ya kwanza kanisa dogo la Moraviani lenye kama washirika 600 lilituma Wamisionari zaidi kuliko kanisa lote la Kiprotestanti kwa miaka 200 iliyotangulia. Miongoni mwa mambo mengine uamsho mwanzoni mwa karne ya 18, uanzishaji wa makanisa ya Moraviani katika nchi nyingi, na mwanzo wa Kanisa a Methodisti linaweza kufuatiwa kwa lindo hili la maombi.

1:6 **Nyumba ya Kimataifa ya Maombi (NYKYM – Jiji la Kansas):** Katikati ya miaka ya 1980 Bwana alimwita Mike Bickle kufuata maisha ya maombi. Alianzisha vikundi kadhaa vya maombi na kuwatia moyo watu kutumia muda zaidi katika maombi kila siku. Baada ya kama miaka 13, vikundi hivi vilianza lindo la maombi ya saa 12 kwa siku na tangu mwaka wa 1999, lindo kamili la maombi ya 24-7-365 lilidumishwa huko katika Jiji la Kansas. Linaitwa Nyumba ya Kimataifa ya Maombi. Kazi ya hawa waombaji ni kuanzisha lindo kama hizi za maombi ulimwenguni mwote. Mike Bickle, na timu inayofanya kazi pamoja naye walibuni kielezo cha maombi kilichoitwa "Kinubi na Bakuli". Kielezo hicho kinaunganisha maandiko, kuabudu, sifa, vita vya kiroho na maombezi katika namna ya pekee (www.fotb.com) Kielezo hiki cha maombi kingeweza kuelezewa kama tanuru la maombi. Katika roho ya Hema Takatifu ya Daudi, maombi yanafanyika saa 24 kwa siku.

1:7 **Nyumba ya Yerusalemu ya Maombi kwa Mataifa Yote**: Nyumba ya Yerusalemu ya Maombi kwa Mataifa yote ilianzishwa na Tom Hess. Mnamo mwaka wa 1987, alienda Yerusalemu kuanzisha lindo la maombi la saa 24 pale ili kuomba kwa ajili ya amani katika Yerusalemu na kwa ajili ya mataifa ya ulimwengu. Malango ya Lindo la Yerusalemu ni sehemu ya uwezo huu wa kuanzisha maombi: timu 12 za maombi huomba kila siku kwa saa 2 kwenye yale malango 12 ya Yerusalemu. Mnamo Septemba 1999, Hess aliitisha mkutano kwa ajili ya lindo za saa 24 ulimwenguni kote. Katika karne iliyopita, lindo zingine kadhaa zilianzishwa huko Israeli (www.jhophan.org/jhophan@jhphan.org).

1:8 **Poland 24:** Poland 24 ni lindo taifa ambapo zaidi ya majiji/miji 50 na sharika kadhaa kila moja ikichukua siku moja kwa mwezi ili kuomba 24/7.

1:9 **Lindo la Maombi Marekani/DC, Washington DC, Marekani:** Mnamo mwaka wa 1998 kikundi cha viongozi wa kitaifa wa Kikristo walipanga juma a maombi ya saa 24 kwenye mahali pa kimkakati huko Washington, DC. Matokeo yalikuwa ya kutia moyo. Viongozi walihisi kwamba Bwana aliwataka kuendelea kukaza juu ya maombi, lakini hawakuweza kufikia kutimiza wito huu. Hata hivyo, mnamo mwaka 1997, wito mpya wa maombi ulitolewa na Lindo la Maombi ya Marekani/DC lilianzishwa kama lindo la taifa la maombi ili kuomba kwa ajili ya Marekani saa 24 kwa siku, kwa lengo maalum juu ya Washington DC, Rais na jukumu la kimkakati la Marekani katika mpango wa Mungu kwa ulimwengu. Kalenda kuu ya maombi inabuniwa ikiwa na majina ya mtu mmoja mmoja na vikundi vya maombi vilivyojitoa ili kuomba kwa saa mahususi kila juma, au kwa angalau saa moja kwenye muda mahsusi mara moja kwa juma. Kwa sasa (2005), zaidi ya waombezi milioni 3 wanahusika katika lindo hili la maombi.

1:10 **Minara ya Maombi huko Indonesia:** Kupitia kazi ya mtandao wa maombi wa taifa huko Indonesia, minara ya maombi imeanzishwa katika zaidi ya miji 500. Kuna minara ya maombi katika miji mingi na kwa wastani waombaji 16 au zaidi watawajibika kwa mnara wa maombi kama huo ili kuomba katika lindo hizi. Watachukua zamu ya saa nne kwa siku. Wakati wa juma watu wengine wanaopenda kuomba (mtu mmoja mmoja na vikundi) pia wanakuja kwenye minara ya maombi ili kuchukua zamu. Wakati mwingine waombezi wanakaa kwa mwezi au zaidi kabla wengine hawajaja kwa kipindi cha muda kama ule ili kuwabadili. Hata watoto (miaka 4-14) wanahusika kuomba katika minara hii ya maombi.

1: 11 **Lindo za Maombi kwa watawaliwa wa madawa ya kulevya**: Mke wa Mchungaji kutoka Pretoria, Afrika ya Kusini, ambaye mwanawe alikuwa ametawaliwa na madawa ya kulevya, alikataa kukata tamaa juu ya mtoto wake na akaanza kuomba kwa bidi sana. Mwaka wa 2001 alikutanisha kikundi cha wazazi kila Ijumaa ya mwisho ya mwezi ili kuomba usiku kucha kwa ajili ya watoto wao waliokuwa wakihusika na kutumia vibaya madawa ya kulevya. Kwa kipindi cha miaka mitatu (2001 – 2004), kikundi hiki cha usiku kucha kilikuwa hadi kufikia minyororo 36 kama hiyo ya maombi ya 24/7/365 ambayo huomba kwa ajili ya watoto amabo wametawaliwa na madawa ya kulevya. Kwa sasa (Sept. 2006), tayari kuna lindo 288 kama hizo za 24/7/365 zinazoombea vijana wanaohusika na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya na mizungu. Kati ya hizo lindo 288, zaidi ya 50% zinaendeshwa kwa saa 24 kwa siku. Watu 12,000 wanahusika na lindo hizi.

1: 12 **Vyumba vya maombi katika makanisa:** Mwaka 1990 Mchungaji Terry Tackle (Marekani) alianzisha chumba cha maombi cha saa 24 kwa siku katika kanisa lake. Ilifanikiwa sana na tangu hapa Tackle alikuwa akihusika kikamilifu katika kuanzisha dhana hiyo katika Marekani yote na pia katika nchi zingine ulimwenguni.

1: 13 **Miji kumi na tano katika mzunguko wa maombi wa majuma 15**: Katika eneo la vijijini la moja ya majimbo ya Afrika ya Kusini, kikundi cha waombezi kiliomba usiku-na-mchana siku 31 za mwezi Mei 2004. Baada ya hapo, wliiendea miji midogo 15 ili ishiriki katika lindo la maombi la usiku-na-mchana. Miji mitatu ilijigawia juma la saa 168 kati yao na kuchukua wajibu kwa ajili ya kipindi cha maombi ya 24-7 kila juma la tano. Hivi sasa wanashughulika sana kuanzisha lindo za maombi sawa na hizo katika maeneo mengine manne.

1: 14 **Kitongoji/Kambi ya wavamiaji ikikolezwa na lindo za maombi:** Mchungaji katika kitongoji (kambi ya wavamiaji) kinachoitwa Shamba la Michungwa, chenye wakazi milioni 1.3, kusini mwa Soweto huko Afrika ya Kusini, alikuja na wazo la kukoleza kabisa kitongoji chote kwa lindo za maombi. Kitongoji hicho kimegawanyika katika mikondo 10 na inajiumuisha miji 10 midogo zaidi iliyoizunguka. Mchungaji huyo alianzisha lindo za maombi katika sekta zote 20 na moja. Hivi sasa lindo za maombi 62 zilizo katika misingi ya sharika zinafanya kazi (angalau 25 kati ya hizo tayari zinaomba kwa saa 24 kamili kwa siku), zikihusisha 40% ya makanisa yote katika kitongoji hicho. Polisi wanatoa taarifa kwamba kwa miezi 6 iliyopita uhalifu ulipungua kwa kiwango cha 20% kwa mwezi. Kuna mtiririko thabiti wa watu wanaompokea Bwana Yesu kama Mwokozi wao. Wanaona uponyaji mwingi, urejezo wa ndoa na mahusiano ya familia pamoja na ukombozi kutoka kwa mapepo.

1: 15 **Vijana na 24/7:** Wendo wa maombi wenye nguvu sana ni ule ulioanza mwa 1999. Mnamo mwezi wa Septemba 1999, Pete Greig aliwapa changamoto vijana 200 wa kanisa katika mji mdogo wa Chichester, karibu na Southampton huko Uingereza, kuomba kwa ajili ya wenzi wao kwa saa 24 kwa siku kwa siku 30. Waliomba mchana na usiku kwa zaidi ya miezi mitatu. Ilipofika Desemba 1999, wendo mpya wa maombi ulikuwa umekwisha anzishwa. Wakati huu (2005), wendo huo unajulikana miongoni mwa vijana kama 24-7. Vikundi vya vijana vinapamba kwa ubunifu mahali pa kukutania ili kutmika kama chumba cha maombi na kisha kuanza kuomba pale kwa saa 168, kwa kawaida kuanzia Jumatatu hadi Jumapili. Kwa upande mwingine lindo la maombi linaachwa wazi kwa majuma kadhaa. Lindo hizi za maombi zinapokuwa za 24-7-365, zinaitwa Vyumba vya Bwela. Inakuwa kawaida zaidi na zaidi kusema 24-7 kama

Chumba cha Bwela. Mwanzoni mwa mwaka 2006, tayari kulikuwa na nchi 65 ambapo wendo huu wa 24-7 umeshika mizizi na unakuwa (www,24-7 prayer.com).

1: 16 **Madhehebu na Mashirika ya Kikristo:** Kutokana na wendo wa maombi wa 24-7 ambao ulianza miongoni mwa vijana huko Uingereza, mwelekeo mpya ulikuwa pole pole. Awali Jeshi la Wokovu huko Australia na kisha huko Uingereza uliomba 52 ya matawi yao kuomba 24-7 kwa juma. Takriban mara moja matawi haya yaishuhudia kwamba hali katika tawi mahususi ilibadilika. Baadhi ya matawi yaliarifu kwamba idadi ya watu waliotubu ilikuwa mara tatu na kwamba makuzi yasiyo ya kawaida yalikuwa yanatokea. YWAM, ikiwa na vituo 16 huko Ulaya Magharibi, lilitenga mwaka mzima ambamo kila kituo kwa zamu kilichukua wajibu kwa juma na kujaza mwaka mzima kwa maombi ya 24-7. Mwanzoni mwa mwaka 2005, kulikuwa na madhehebu na mashirika ya Kikristo 13 huko Uingereza peke yake ambayo yalianza kujaza mwaka mzima na maombi ya 24-7.

1: 17 **Milima ya Maombi:** Korea ya Kusini inajulikana sana kwa milima ya maombi. Madhehebu mbalimbali yalianzisha mahali pa kukutania katika milima ambapo watu wanaweza kwenda na kuomba usiku-na-mchana. Nyingi ya sehemu hizi za kukutania zinatoa makao ya kutosheleza, yana kanisa dogo, kambi za mihadhara, vituo vya maombi na vijichumba vya maombi ambamo mtu mmoja mmoja huweza kuomba peke yake. Mara nyingi Wakristo huenda pale ili kuomba (na pia kufunga) kwa vipindi hadi siku arobaini. Katika mingi ya milima hii ya maombo kuna mtiririko endelevu wa wagni ambao wanakuja kuomba. Wanaombea masuala ya binafsi, na pia kwa ajili ya nchi, Korea ya Kaskazini, na kwa ajili ya ulimwengu. Kulingana na kanisa huko Korea ya Kusini, uhifadhi na uthabiti wa kisiasa huko Korea ya Kusini, pamoja na makuzi ya kanisa katika nchi, yanaweza kuhesabiwa kwenye maombi yanayofanyika katika sehemu hizi za kukutania huko milimani.

1: 18 **Lindo za maombi za Neno:** Katika siku zile 10 za maombi ya usiku-na-mchana ya 6-15 Mei 2005, kanisa huko Pretoria, Afrika ya Kusini, lilianzisha lindo tatu za maombi ambazo kila moja liliomba kutoka kwenye Maandiko tu. Katika chumba cha kwanza cha maombi waombaji walisoma Biblia kutoka Mwanzo hadi Ufunuo na kuomba kwa saa 240. Katika chumba cha pili cha maombi walisoma Zaburi, maombi ya Yesu na maombi mengine kadhaa katika Agano la Kale. Katika chumba cha tatu cha maombi walisoma majuzuu ya dondoo kutoka kwenye Maandiko (maelfu ya ahadi, amri, maombi ya mitume katika AJ, Maandiko juu ya tabia ya Mungu, na juu ya kusudi la Mungu kwa wanadamu n.k.). Kutoka tarehe 17-23 Oktoba 2005 katika sehemu mia moja katika Afrika ya Kusini

makanisa ya mahali pamoja na vikundi vya makanisa viliungana ili kusoma na kuomba Neno (Kutoka Mwanzo hadi Ufunuo pamoja na Zaburi kwa kurudiarudia) kwa saa 168.

1: 19 **Magereza:** Katika magereza kadhaa huko Argentina Wakristo wameanzisha lindo zenye nguvu za 24/7/365 (yaani Olmosi na Kristo tumaini pekee). Wanawaombea wenzao, familia zao, Jumuiya zao, nchi na ulimwengu. Kuna shuhuda za ajabu za wongofu na mabadiliko ya mtindo wa maisha kutoka kwa wafungwa na aina nyingine za upenyo katika magereza huko Argentina. Matunda mengi ni kwa sababu ya maombi ya usiku-na-mchana. Huko Afrika ya Kusini magereza kadhaa yameomba kwa kurudiarudia usiku-na-mchana kwa vipindi vya siku saba kwa miaka miwili iliyopita.

"Moto utawaka daima juu ya madhabahu, usizimike" (Law. 6: 13).

SEHEMU YA 2:

Sababu za maombi ya usiku-na-mchana.

2:1 Msingi wa Maandiko kwa ajili ya maombi ya usiku-na-mchana.

2:2 Faida ya maombi ya mchana-na-usiku

2:3 Maombi na utendaji

2:4 Uchunguzi mfupi juu ya matumizi ya neno "Lindo" katika maandiko.

2:1 **Msingi wa Maandiko kwa ajili ya maombi ya mchana-na-usiku.** Dhana ya maombi ya usiku-na-mchana imesimama imara katika Maandiko na kanuni kadhaa za Biblia.

1. Mungu anatulinda kwa saa 24 kwa siku (Zab. 121) na katika Neno lake anatuita kukesha na kuomba pamoja naye. Ufunuo 4-5 zinaeleza kwamba malaika na wazee 24 wanamwabudu Mungu kiuhalisi usiku na mchana. Biblia inatufundisha kwamba mapenzi ya Mungu yatendeke duniani kama ilivyo huko mbinguni na huko mbinguni kuna sifa, kuabudu na maombezi tu, saa 24 kwa siku. Njia pekee ambayo hii itaweza kutimizwa, ni kwa kuanzisha lindo za maombi za saa 24.

2. Katika Agano la Kale, moto juu ya madhabahu: *"Na huo moto ulio madhabahuni utatunzwa uwake daima juu yake usizimike; naye kuhani atateketeza kuni katika moto huo kila siku asubuhi; naye ataipunga sadaka ya kuteketezwa juu yake. Moto utatunzwa uwake juu ya*

madhabahu daima; usizimike" (Law 6: 12-13). Majukumu mawili muhimu sana ya kuhani yalikuwa: a) maombezi (kupitia maombi na sadaka); na b) sifa na kuabudu. Moto katika madhabahu ilikuwa ishara ya mwendelezo wa sifa, kuabudu, maombezi na upatanisho unaofanywa na makuhani.

3. Mungu mweyewe anatuteua kama walinzi juu ya kuta ili kuomba kwa ajili ya utimilizo wa ahadi zake: *"Nimeweka walinzi juu ya kuta zako, Ee Yerusalemu; hawatanyamaza mchana wala usiku; ninyi wenye kumkumbusha Bwana ahadi zake msiwe na kimya, wala msiacha akae kimya, mpaka atakapoufanya imara Yerusalemu na kuufanya kuwa sifa duniani"* (Isa 62: 6-7).

   Angalizo: a) Ni Mungu mwenyewe anayewateua walinzi; b) Lazima wasimame mbele zake saa 24 kwa siku; na c) walinzi hawatakaa kimya au kumwacha akae kimya hadi ahadi zake zote ziwe zimetimizwa. Neno la Mungu lina maelfu ya ahadi kwa ajili ya watoto wake na Maandiko yanatuagiza kudumu kuomba kwa ajili ya utimilizo wa ahadi hizi.

4. Katika Luka 18: 7 Mungu anaahidi kwamba atatupatia haki (kuweka sawa kilichokosa – uhalifu, vurugu, matumizi mabaya ya madawa ya kulevya rushwa, ufisadi, udhaimu, ndoa zilizovunjika na ugonjwa wa mlipuko wa UKIMWI) kama tutamwita usiku-na-mchana. *"Na Mungu je!. hatawapatia haki wateule wake wanaomlilia mchana na usiku, naye ni mvumilivu kwao?* (Lk. 18: 7).

5. Nyaraka za Paulo mara nyingi zinasemea juu ya maombezi ya mchana-na-mchana kwa ajili ya kanisa na maendeleo ya Injili.

6. Kumtumikia Mungu Baba usiku na mchana kupitia sifa na kuabudu, kukua katika uhusiano wa karibu na Mungu na kuishi katika sura yake. Ufu 4: 8-11*: "Na hawa wenye uhai wanne, kila mmoja alikuwa na mabawa sita; na pande zote za ndani wamejaa macho (chini ya mbawa zao), wala hawapumziki usiku na mchana, wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi, aliyekuwako na aliyeko na atakayekuja. Na hao wenye uhai wanapompa yeye aketiye juu ya kiti cha enzi utukufu, na heshima na shukrani, Yeye aliye hai hata milele na milele; ndipo hao wazee ishirini na wanne huanguka mbele zake yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi, nao humsujudia yeye aliye hai hata milele na milele, nao huzitupa taji zao mbele ya kile kiti cha enzi, wakisema, Umestahili wewe, Bwana na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa*

wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa".

7. Kukiombea kizazi hiki cha vijana ili kimrudie Mungu na kuwa wanaume na wanawake wanaomcha Mungu watakaotekeleza Agizo Kuu na Amri Kuu. Omb. 2: 18 – 19: *"Mioyo yao ilimlilia Bwana; Ee ukuta wa Sayuni, Machozi na yachuruzike kama mto usiku na mchana, usijipatie kupumzika, macho yako yasikome kutoa machozi. Inuka, ulalamike usiku, mwanzo wa makesha yake; mimina moyo wako kama maji usoni pa Bwana; umwinulie mikono yako; kwa uhai wa watoto wako wachanga wazimiao kwa njaa, mwanao wa kila njia kuu".*

2:2 **Faida ya maombi ya usiku-na-mchana**

1. Lindo la maombi ya 24-7 litakuwa njia moja ambayo kanisa linaweza kutimiza amri ya Mungu ya kuwa nyumba ya maombi kwa ajili ya mataifa (Isa 56: 7). Kwa kutekeleza lindo za maombi ya 24-7, makanisa yanaweza kuchukua wajibu na kusimama kama walinzi juu ya kuta kwa ajili ya kanisa duniani kote, kwa ajili ya jumuiya zao, nchi yao na kwa ajili ya mataifa mengine.

2. Sifa, kuabudu na maombezi ya saa 24 yanasababisha kipimo kipya na cha kina kuhusu uhusiano wa mwombezi na Mungu.

3. Lindo la maombi la saa 24 linalenga kuleta mavuno.

4. Kupitia lindo za maombi tunaweza kuomba usiku-na-mchana kwa ajili ya mahitaji yetu na maombi ya jumuiya.

5. Maombi ya usiku-na -mchana yanatusaidia kustahimili katika maombi, ili kuendelea kwenye maombi na kuomba daima kama Neno linavyotuagiza kufanya hivyo.

6. Lindo la maombi la saa 24 linakuza umoja miongoni mwa waumini kwa sababu wanalenga juu ya masuala yale yale na kuyaombea pamoja. Pia linaunganisha pamoja makanisa na madhehebu.

7. Yanasaidia kila mwombezi na kikundi cha maombi kuelewa kwamba wana wajibu na inawatia nguvu kujua kwamba hawaombi peke yao, jambo ambalo kwa watu wengi ni kutiw amoyo sana.

8. Historia inatuonyesha kwamba maombi ya usiku-na-mchana yalikuwa na matokeo makubwa kwa jumuiya na kwa ulimwengu.

2:3 **Maombi na utendaji:**

Maombi yenyewe si mwisho. Maombi yanatuleta kwenye ushirika na Mungu Baba, Yesu Kristo na Roho Mtakatifu. Tunapoanza kuwa na ushirika na Yesu, atatufunulia moyo wake na kutupeleka kwa watu walio katika uhitaji. Kusudi la maombi ni kututia nguvu ili kuiishi Amri Kuu (kupenda…) na Agizo Kuu (kuenenda…). Hatuombi tu kwa ajili ya kuomba. Maombi halisi siku zote yataongoza kwenye utendaji: kugusa maisha ya watu kwa upendo na huruma ya Kristo.

1. Maombi siku zote lazima yaongoze kwenye mtindo wa maisha ya utume – kuchukua upendo na wokovu wa Yesu kwa watu wenye uhitaji wa wokovu, faraja na uponyaji.

2. Ili kujenga juu ya msingi wa maombi, ni lazima tuishi kama wanafunzi wa Yesu, tukimfuata yeye popote aendapo bila kujali gharama.

3. Maombi lazima yaongoze kwenye maisha ya huruma kwa wote wenye uhitaji.

4. Maombi yanafanya msingi kwa ajili ya Wakristo kuishi katika amani, upatanisho na katika upendo wa mtu na mwingine.

5. Maombi yanatuleta kwenye maisha ya uhusiano wa karibu na Yesu.

6. Kupitia maombi tunapokea nguvu kutoka kwa Mungu (kupitia Roho Mtakatifu) ili kuwa mashahidi wa upendo, wokovu na huruma ya Yesu na kuchukua hadi miisho ya dunia.

   Baadhi ya watu huomba ili tu kuomba na baadhi ya watu homba ili kumjua Mungu – Andrew Murray.

2:4 **Uchunguzi mfupi juu ya matumizi ya neno "lindo" katika Maandiko**.

Katika Mwa. 2: 15 Mungu alimteua mwanadamu kuwa mwakilishi wake, watu kama walinzi, waangalizi wa Bustani ya Edeni. Neno la Kiebrania kwa ajili ya "lindo" ni ***shamar,*** moja ya maneno matatu yanayotumiwa kwa ajili ya mlinzi katika Agano la Kale. Adamu aliambiwa kuiangalia ile bustani na kuitunza. Meneno mengine mawili ni ***natsar na tsaphah*** – Maneno yote haya matatu ya Kiebrabua yanamaanisha ulinzi na kukinga, pamoja kitendo cha shari na kushambulia. Kwa hiyo tunaweza kusema kwamba maneno haya kwa uhalisi yanamaanisha kulinda au kuhami kwa kuweka lindo, kuhifadhi au kuficha.

Maneno mawili ya Kiyunani kwa ajili ya "kulinda" ni ***gregoreuo*** na ***agrupneo***. Yote yanamaanisha ulinzi, lakini kwa dhahiri yanamaanisha "kuwa macho au kutokuwa na usingizi". Maneno hayo yanahusisha mshika gadi, skauti, mlinzi wa usiku – mtu ambaye jukumu lake ni kukaa macho, kuwa katika tahadhari kwa ajili ya dalili za hatari.

Katika nyakati za Agano la Kale, mlinzi alikuwa anawajibika kwa a) kutunza mazao; na b) kuweka lindo kwa ajili ya maadui juu ya kuta za jiji. Wakati wa mavuno (pia kwa maana ya kiroho), huduma za mlinzi ni muhimu. Ulimwenguni kote sasa ni wakati wa mavuno, ndiyo sababu kwa sasa tunahitaji walinzi – ili kulinda mavuno ya Mungu (Yn 17: 12) na kuyahifadhi. Walinzi, hata hivyo, waliwekwa juu ya kuta za miji ili kuwalinda watu wake na kuhakikishia usalama (Isa 1: 6-8, Isa 62: 6; Eze 22: 30). Na hawa wenye uhai wanne … hawapumziki usiku-na-mchana wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi (mweza yote), Aliyekuwako na Aliyeko na Atakayekuja… (Ufu 4: 8-11).

Omba mara kwa mara; kwa kuwa maombi ni ngao ya nafsi, dhabihu kwa Mungu na kiboko cha shetani – John Bunyan.

SEHEMU YA 3:

Miongozo ya jumla:
3:1 Mahali pa kukutania panapotumiwa kwa ajili ya lindo za maombi.
3:2 Mitazamo mbalimbali ya kuwafanya watu wahusike.
3:3 Idadi ya marudio ya kuhusisha
3:4 Majina mbalimbali yanatumiwa kwa ajili ya lindo za usiku na mchana
3:5 Lengo la maombi ya lindo za maombi
3:6 Tovuti za kusaidia

3:1 **Mahali pa kukutania panapotumiwa kwa ajili ya lindo za maombi.**
Ulimwenguni pote watu wanatumia karibu kila aina ya mahali pa kukutania ili kuanzisha lindo zao. Ifuatayo n mifano ya sehemu za kukutania kama hizo:-

- Nyumbani au maghorofani
- Gereji au ghala
- Vyumba vya nyuma, ghorofa ya juu kabisa au ghorofa ya chini
- Banda
- Kanisa dogo au majengo ya kanisa
- Vyumba vya maombi vilivyowekwa wakfu
- Ofisi au mahali pa kukutania kwenye kituo cha manunuzi/dukani
- Ndani ya magereza

3:2 **Mitazamo mbalimbali ya kuwafanya watu wahusike:**

- Watu kadhaa mmoja mmoja wenye nia sawa watachukua saa moja kila mmoja kujaza zile saa 24
- Kanisa la mahali pamoja litajitoa kwa kujifunga ili kumaliza juma 24/7
- Makanisa kadhaa ya mahali pamoja yataungana: Kila kanisa kwa mfano litachukua siku moja kwa juma na kwa njia hiyo wanaanzisha lindo la 24/7/365
- Jumuiya inaweza kuamua kwamba wanahitaji lindo la 24/7. Mtu mmoja mmoja, makanisa ya mahali pamoja, vikundi vya maombi na vikundi vya vjana vitaungana kukijaza chumba kama hicho kwa maombi 24/7
- Vijana katika sekondari/sekondari ya juu au vyuo vikuu/vyuo wanajitoa kwa kujifunga ili kuanzisha lindo la 24/7 kwenye kampasi yao
- Watoto (umri wa miaka 6-14) wakati mwingine wanahamasishwa kwenye lindo za maombi. Wanachukua nafasi katika lindo lililoanzishwa au atajitoa kwa kujifunga kuchukua saa kadhaa kwa juma
- Idadi inayokua ya watu ulimwenguni kote watajitoa kwa kujifunga kwa vipindi vya muda (miezi michache, mwaka au muda mrefu zaidi) ili kutumika kwa msingi wa muda wote kama wamisionari wa maombi katika lindo la maombi

3:3 Marudio ya kuhusika

- Baadhi ya watu mmoja mmoja watataka kuomba saa moja kwa siku
- Baadhi wataweza kuja mara moja kwa juma au mara moja kwa wiki mbili
- Wengine watakuja mara kwa mara
- Baadhi watakuja kwa nafasi za saa moja, wengine hutumia nafasi za saa mbili au nafasi za dakika 30
- Watoto wanaweza kutaka kuchkua nafasi za dakika 10-15
- Baadhi ya lindo zitaomba kanisa la mahali pamoja kuomba kwa siku moja kwa juma au siku moja kwa mwezi
- Baadhi ya lindo hazina utaratibu kabisa na watu watakuja na kuondoka kwa kutaka wenyewe, wengine wana nidhamu sana na wanatazamia washiriki wawahi na kufanya nafasi mahususi

3:4 **Majina mbalimbali yanatumiwa kwa ajili ya lindo za maombi za usiku-na-mchana.**

- Minyororo ya maombi
- Vyumba vya maombi

- Nyumba za maombi
- Vyumba vya bwela
- Lindo za 24/7
- Minara ya maombi
- Nyumba za nguvu
- Milima ya maombi

3:5 **Lengo la maombi ya lindo za maombi**

Lindo za maombi zinaanzishwa kwa sababu na makusudi makubwa mbalimbali, kwa mfano:-

- Kama vituo vya kusifu na kuabudu
- Maombezi na maombi ya vita
- Kuomba Neno la Mungu (yaani Lindo la Maombi la Ulimwengu, Mji wa Rasi, Afrika ya Kusini)
- Kwa ajili ya maombi ya faragha, kimya, kutafakari na ya kisufii (yaani Taize huko Ufaransa)
- Muunganiko wa kuabudu, maombezi na vita (yaani Nyumba ya Kimataifa ya Maombi huko katika Jiji la Kansas, Marekani)
- Kuomba kwa ajili ya mataifa ya ulimwengu
- Kuomba kwa ajili ya mahitaji ya msingi ya jumuiya
- Kuomba kwa ajili ya taifa: uamsho, uchumi hali ya kisiasa n.k.
- Kuomba kwa ajili ya Kanisa la mahali pamoja
- Muunganiko wowote wa hayo ya hapo juu

3:6 **Tovuti za kusaidia**

www.global24-7.com
www.24-7prayer.com
www.fotb.com
www.jwipn.com
www.xtremeprayer.com
www.ipcprayer.org
www.globaldayofprayer.com
- http://www.global24-7/com

"Kwa maana macho ya Bwana hukimbia kimbia duniani mwote ili kuwatia nguvu wale waliomwelekea kwa ukamilifu" (2Nyakati 16:9).

Mara nyingi nimepelekwa magotini na kutiwa hatiani kwenye kutisha kwamba sikuwa kabisa na mahali pengine pa kwenda – Lincoln

Watu wanaweza kudharau maombi yetu, kukataa ujumbe wetu, kupinga hoja zetu, kutweza nafsi zetu, lakini wako hoi dhidi ya maombi yetu – J. Sidlow Baxter

SEHEMU YA 4:

Jinsi ya kuendesha chumba cha maombi

4:1 Miongozo ya lindo za maombi za 24-7-365
4:2 Thamani na kanuni kwa ajili ya kujenga lindo la maombi la 24/7/365
4:3 Mwongozo kwa ajili ya kuanzisha lindo la maombi la 24/7 (saa 168)
1. Kanuni za msingi za kukumbuka wakati wa kuanzisha lindo la maombi
2. Miongozo ya ujumla
3. Jinsi ya kuendesha chumba cha maombi cha 24-7
4. Mawazo mengine machache

4:4 Mfano wa chumba cha maombi cha kuingiliana pamoja na vituo vya maombi

4:1 Miongozo ya lindo za maombi za 24-7-365

- Ni jambo moja kufanya lindo la maombi kuendelea kwa siku saba, lakini suala tofauti sana kufanya lindo la maombi kuendelea kwa siku 365, mwaka nenda rudi.

- Awali ya yote ni muhimu kukumbuka kwamba watumishi zaidi wanahitajika ili kufanya lindo la maombi la siku 365 kuendelea
- Pili ni lazima wawepo waombaji wa kutosha waliojiweka wakfu
- Tatu, inahitaji kupanga kwa uangalifu, mwongozo ulio wazi na hamasa

- Timu inahitajika kufanya lindo kama hilo la maombi kuendelea: mratibu mkuu; waratibu wa kila siku ya juma, timu ya utawala na zaidi ofisi ya utawala; timu inayoweza kukusanya nyenzo za maombi, kutayarisha na kufanya zipatikane kwa waombezi katika machapisho au kupitia baru apepe; timu ambayo itawajibika kusafi na kupamba mahali pa kukutania pa maombi, mtu atakayebuni ratiba ya maombi; n.k.

- Ni lazima uwepo mchakato endelevu wa kuandikisha waombezi wapya ili kujiunga na lindo la maombi. Ni lazima wachukue nafasi ya wale wanaohamia miji au majiji mengine au wale wanaochoka na kuacha

- Ni muhimu kuwahamasisha waombaji mara kwa mara ili waendelee na kuwatayarisha kwa ajili ya maombi ya nguvu. Kumbuka kwamba baadhi yao hushiriki katika lindo la maombi kama mtu mmoja

mmoja au washirika wa vikundi vidogo vidogo, na kwamba si lazima wawe na mawasiliano na waombaji wengine. Waombaji wanaweza kuwa urahisi kujisikia wametengwa na kisha kuvunjika moyo.

4:2 Thamani na kanuni kwa ajii ya kujenga lindo za maombi za 24/7/365

- Elekeza maono ya maombi ya usiku-na-mchana na uendelee kuelekeza maono hayo siku kwa siku, juma kwa juma. Watu wanahitaji maelekezo na kutiwa moyo.
- Viongozi (pia viongozi wa lindo la maombi) ni lazima waamini katika nguvu na ulazima wa maombi.
- Maombi ni lazima yatolewe kielelezo na uongozi wa kanisa
- Weka mkakati kwa uangalifu na unganisha shughuli zilizopo za maombi ili kuanza 24/7.
- Naibisha au gawa wajibu kwa uangalifu kadiri lindo linavyokuwa, utahitaji watu mmoja mmoja wenye karama mahususi ili kusaidia kukidhi mahitaji yanayokua ya kivitendo na kiroho ambayo yanaweza kutokea. Utahitaji kwa mfano mtu mwenye ujuzi mkubwa wa kiutawala na kuratibu.
- Unganisha 24/7 na huduma mbali mbali katika kanisa
- Weka rahisi – Ni mkakati rahisi ambao unafanya maombi yawe rahisi. Wajibu wa msingi kabisa ni kuomba na kuita watu kwenye maombi
- Endelea kuwasiliana na kuwapa watu taarifa ya maombi – tumia nyenzo na nyaraka zilizoko za maombi zenye wito wa Kibiblia wa maombi
- Shikilia thamani ya umoja katika Roho Mtakatifu
- Elewa shinikizo la jamii ya kisasa – tumeitwa kuwatia moyo watu kuomba na siyo kuwashinikiza. Fanya iwe rahisi kwa mtu mmoja mmoja kujiunga na usiwakosoe kama hawatafanya hivyo. Haitufanyi kuwa Wakristo bora zaidi kwa sababu tu tunaomba zaidi kuliko wengine. Baadhi ya watu wanaweza kuomba kwa saa nyingi wakati wengine wanaweza kuomba kwa nusu saa tu.
- Tilia mkazo umuhimu wa ibada za binafsi na ibada za familia. Kuomba katika lindo la maombi kamwe yasichukue nafasi ya muda wako binafsi wa pekee na Mungu.
- Uwe mbunifu na kujitayarisha kwa mabadiliko – soma na sikiliza. Kuhusisha vijana kunahitaji hata ubunifu zaidi.
- Toa nafasi na ubunifu fursa kwa ajili ya kuwafundisha na kuwatayarisha waombezi. Watu pia wanahitaji mafundisho ya kivitendo juu ya jinsi ya kuomba.
- Kuwa nyumba ya sala siyo changamoto – ni amri ya Kibiblia (Mt. 21: 13).

- Toa nafasi kwa ajili ya wale walioitwa kwa huduma ya kudumu katika nyumba ya maombi. Bwana anawainua walinzi wa kudumu ulimwenguni kote wenye wito wa msingi ndani ya nyumba ya maombi. Kunaweza kuwa na baadhi ya wanaume na wanawake hawa katika usharika wako ambao watatafuta kuhudumu mbele za Mungu kila siku katika kufunga na kuomba kama Ana katika Agano Jipya (Lk. 2: 37).
- Hakikisha unajenga kwa upana pamoja na kina zaidi – wendo wa maombi unakuwa kwa upana na kina zaidi. Wendo wa maombi wa 24/7 unatoa chombo kwa ajili ya wale wanaotaka kukuza maisha ya maombi ya kina zaidi na Mungu.
- Funguo 3 ya kukumbuka katika kuhimili lindo la usiku-na-mchana: a) nidhamu ya binafsi b) uvumilivu c) kujitoa binafsi kwa kujifunga (kuchukua nafasi yako ya maombi).

4:3 **Miongozo kwa ajili ya kuanzisha lindo la maombi la siku 7 (saa 168).**

Kanuni za msingi zifuatazo lazima ziwekwe maanani wakati wa kuanzisha lindo la maombi: Siku zote lazima kanisa la mahali pamoja lazima lichukuliwe kwa heshima ya juu. Kama utapenda kuaanzisha lindo la maombi la saa 24, lifikirie kanisa la mahali pamoja kama jiwe kuu la msingi. Makanisa ya mahali pamoja ni lazima yawe nyumba za maombi.

Kanuni za msingi za kukumbuka wakati wa kuanzisha lindo la maombi:

- Katika lindo la maombi Neno la Mungu lazima lifaidi umuhimu wa kwanza. Maombi mengi yapo katika msingi wa kdondoo na shauku binafsi. Ahadi za Mungu zinafunuliwa kwetu katika Neno lake, na Neno linatufundisha mapenzi yake ni yapi. Ndiyo maana ni muhimu kwamba waumini waanze kuomba Neno tena.
- Aina nne za msingi sana za maombi ni kusifu/kuabudu, ungamo la dhambi, maombezi, na kushukuru. Kusifu na kuabudu kunatambua utawala wa Kristo na kumtukuza. Ungamo la dhambi huondoa vizuizi kati ya Mungu na sisi. Maombi ya maombezi ni ombi kwa ajili ya Mungu kuingilia kati katika hitaji/mahitaji ya watu. Madokezo haya yote ni muhimu katika lindo la maombi.

- Kwanza, lindo za maombi hazikusudiwi kuwa kwa ajili ya kuombea mahitaji binafsi. Wakati wa lindo la maombi, lengo ni juu ya mahitaji yakanisa/jumuiya/jiji la mahali pamoja na ulimwengu kwa ujumla.

- Usikimbilie kwenye lindo la maombi la 24/7/365. Anza na siku moja kwa juma, saa arobaini kwenye mwisho wa juma au juma la maombi ya usiku na mchana (saa 168). Rudia hivi mara chache na ndipo tu uanze kupanga lindo la maombi la 24/7/365. Wakati mwingine mtu anajisikia kuvuviwa kiasi kwamba unataka kuendelea kuomba "hadi Yesu aje tena!".

2. Miongozo ya ujumla:

- Lindo au mnyororo wa maombi wa siku 7 unaweza kuhusisha mtu mmoja mmoja, vikundi, makanisa, miji/majiji au mikoa/majimbo.
- Makanisa yanaweza kuanza na lindo la maombi la siku moja saa 24 mara moja kwa juma na jinsi watu wengi wanavyohusika, siku zaidi zinaweza kutumiwa katika maombi. Mara wanapokuwapo waombezi wa kutosha kujaza saa zote za siku moja, mnyororo unaweza kutiwa nguvu kwa kuanzisha mnyororo wa pili ambao unafanya kazi kwa siku ile ile. Saa katika lindo la maombi zinaweza kuchukuliwa na mtu mmoja mmoja, vikundi vya maombi, vikundi vya vijana, vikundi vya seli, n.k.
- Kila kanisa linaweza kushirikiana na kanisa lingine, au makanisa mengine kadhaa kuwatia moyo pia kuanzisha lindo la maombi la 24-7 (saa 24 kwa siku kwa siku 7). Tia moyo makanisa, vikundi vya maombi baina ya madhehebu na mashirika ya Kikristo kwa kila moja kuchukua sehemu kubwa ya siku saba (saa 168) ili kuomba kwa saa 24 kwa siku, na kisha kuanzisha lindo kama hizo za 24-7 katika jumuiya zao angalau mara mbili au tatu kwa mwaka. Kanisa au kiasi cha makanisa (hata kufikia makanisa au vikundi 20 au 30) yanaweza kuchukua siku kwa juma, katika mwaka mzima ili kuomba kwa saa 24. Shirikiana na makanisa mengi kwa kadiri inavyowezekana kuanzisha lindo la maombi la 24-7 ndani ya eneo au mkoa fulani. Mwanzoni si makanisa yote yataweza kuwajibika kwa saa zote 24 kila juma. Kwa hali kama hizo, anza na saa 6, 12 au 18. Makanisa mawili au matatu yangeweza, kwa mfano, kila moja kuchukua kiasi cha saa kwa siku fulani na hivyo kujaza saa zote 24.
- Lindo la maombi la 24-7 litakuza uelewa wa hitaji la kumaanisha kwa ajili ya maombi. Upenyo wa kiroho katika jumuiya kwa kawaida hufuata uanzishaji wa lindo za maombi.
- Zaidi ya kutumia kanisa la mahali pamoja kama jiwe la msingi la kujengea kwa ajili ya kuanzisha lindo za maombi za saa 24, njia/vielelezo vingine vinaweza pia kutumiwa ili kutia moyo maombi ya 24/7.
- Vikundi vinaweza kila kimoja kuwajibishwa kwa saa moja ya maombi. Toa mwanya kwa baadhi ya vikundi kuomba kwa saa mbili kwa wakati. Kama kwa kuanzia saa 24 ni ndefu sana, anza na mnyororo wa saa 12 au 18.
- Tena mratibu na mratibu msaidizi kwa kila mnyororo wa saa 24.
- Lindo la maombi linaweza kufanya kazi kwa njia mbili
- Tafuta mahali pakuu pa kukutania kanisani au penginepo panapopatikana kwa saa 24 kwa siku, ambapo watu wanaweza kukutana ili kuomba, au

b) achia mtu mmoja mmoja au vikundi kuamua ni wapi wanapenda kukutana kwa ajili ya saa yao ya maombi (kwa mfano, nyumbani kwao).

Miongozo hii ni mapendekezo tu. Uwe mbunifu. Roho wa Bwana anaweza kukuongoza kuendea suala hilo katika njia tofauti kabisa. Hakuna njia sahihi au ya makosa ya kuomba.

3. Jinsi ya kuendesha chumba cha maombi cha siku 7.

- Kipindi cha maombi cha siku 7 kinaweza kuendelea kutoka usiku wa manane Jumapili hadi usiku wa manane Jumapili inayofuata.
- Mlango wa chumba cha maombi uachwe wzi usiku na mchana. Chumba cha maombi kitoe mahali ambapo washiriki wa kanisa au jumuiya wanawza kukutana uso kwa uso na Mungu, kuhisi uwepo wake na kusema naye juu ya mahitaji ya ulimwengu. Kitabu cha mwongozo cha 24-7 (kinachoitwa Kitabu cha mwongozo cha Chumba cha Bwela – hususan kwa ajili ya vijana) kinapatikana katika www.xtreamprayer.
- Tafuta chumba, au nafasi, na ugeuze iwe chumba cha maombi kwa siku saba. Chumba mahsusi cha maombi ambacho watu wanaweza kuja kinafanya kazi kwa ubora zaidi. Uwe thabiti na uwatie watu moyo ili waje kwenye chumba cha maombi kuomba!.
- Weka mpango salama kama ni lazima.
- Kama makanisa kadhaa yatashiriki katika 24-7 moja, chumba cha maombi kisiwe kwenye moja ya makanisa yanayohusika. Mahali pa kukutania pasipohusika na upande wowote panapendekezwa.
- Hakikisha kwamba vyoo vinafunguliwa 24-7
- Gawanya chumba cha maombi katika sehemu mbalimbali ambazo watu wanaweza kukaa na kuomba. Ita sehemu hizi vituo vya maombi (au kuta za maombi) na uwaelezee wageni kwamba wanaweza kutulia ili kuomba katika kituo chochote wakati wowote. Watu ambao wanaweza kupiga chombo cha muziki wanaweza kumsifu Bwana kwenye Ukuta wa Sifa, au mtu mwingine anaweza kucheza CD. Inaweza kuwa wazo jema kuweka sehemu kutoka kwenye maandiko juu ya ahadi za Mungu katika ukuta wa Ahadi ili kwamba waombezi waweze kusimama pale pale na kuomba Maandiko. Buni Ukuta wa Asante au pembe ambapo watu wanaweza kubandika shuhuda za maombi yaliyojibiwa na vidokezi vya shukrani. Ukuta wa Kuomboleza ni wazo zuri pia; majina ya wahitaji na matakwa mengine ya maombi yanaweza kubandikwa pale. Vituo vya treni na sehemu maarufu sana kwa wasanii wa grafiti (michoro ya mikwaruzo/maneno ya ukutani) hivyo buni Ukuta wa Grafiti ambako watu wanaweza kuandika mashairi ya kiroho, nyaraka na mithali, au kujieleza katika michoro. Tazamia kwamba utomvu wa ubunifu utaanza kutiririka watu watakapoomba kwa makini na kubandika makaratasi makubwa ukutani kwa ajili yao kuandika. Weka kiasi cha mito sakafuni ambapo watu wanaweza tu kuwa kimya na kutumia muda na Bwana.

- Hakikisha mara mbili kwamba kuna kalamu, karatasi, penseli za rangi na rangi za kuchorea katika chumba cha maombi. Inasaidia kama mtu anaweza kuandika au kutoa kielelezo cha maombi yako na kubandika juu ya ukuta.
- Toa kahawa, chai na maji ya kutosha.
- Maombi ya kivitendo ya nje ya vituo: Endesha hadi kwenye shule, kituo cha polisi, kituo cha manunuzi, kituo cha teksi au gulio la karibu na omba papo kwa papo kwa ajili ya watu wanaofanya kazi pale. Unaweza kujenga kibanda pale kwa siku moja au saba, ili kwamba watu wanaohitaji maombi wanaweza kukuomba uwaombee.
- Kumbuka, jukumu hili ni kubwa sana kwa mtu mmoja kutekeleza, hivyo omba watu wachache wenye karama ya utawala ili kusaidia katika utekelezaji wa kivitendo wa juma lako la maombi.
- Waombe watu wachache wa kujitolea ili kusaidia usafiri, hususan kuwapeleka watu kwenye chumba cha maombi usiku.
- Omba na yule mwombezi anayechukua zamu yako
- Jumuisha timu za kuabudu na kusifu katika ratiba hiyo na alika timu hizi kuchukua saa mbili kwa wakati kumsifu na kumwabudu Bwana kwenye mahali pako pa kukutania
- Fanya mpango kwa ajili ya wazee na mama vijana wenye watoto kuja kwa vikundi wakati wa mchana, na kwa vijana kujaza mahali pale kwenye mwisho wa juma. Vijana wanaweza kukaa usiku kucha Ijumaa au Jumamosi jioni. Waruhusu wale wenye kusinzia kuleta mifuko yao ya kulalia lakini ninaweza kwa kiasi kikubwa kukuhakikishia kwamba hawatatumia.
- Tia moyo vikundi vya vijana (au wazee), vikundi vikubwa vya maombi, sharika au makanisa ya mahali pamoja katika eneo kuanzisha pamoja 24-7.
- Huduma za kuwafikia wahitaji: Watu wanaokuja kuomba katika juma, wanaweza kuombwa kuleta nguo, chakula, samani au mablanketi ili kuwapa wahitaji. Wakati zawadi inapotolewa, ombea familia unayotolea. Wabariki katika Jina la Yesu.

4. Mawazo mengine machache:
    - Huenda ni muda wa kutoa changamoto kwa shule ya mahalipamoja kuomba kwa siku 7. Wazazi wanaweza kujaza ratiba hiyo wakati wa saa za shule, na wanafunzi wanaweza kuwajibika kwa ajili ya alasiri na jioni.
    - Kichukue kikundi cha vijana kwenye tukio lisilo la kawaida – lindo la maombi la saa 40 mwisho wa juma kutoka saa 12 jioni Ijumaa hadi saa 6 adhuhuri Jumapili.
    - Pata makanisa machache kufanya kazi pamoja ili kuomba usiku na mchana kwa juma zima.

- Chukua dhana ya 24-7 kwenye "mahali pa giza" mwisho wa juma au wakati wa sikukuu na omba kwenye ngazi ya mlango wa adui. Wakati huo huo unaweza kuwaambia juu ya upendo wa Yesu.
- Wanaume au wanawake waliojiweka wakfu wanaweza kuchukua muda kwenda kwenye faragha. Badala ya kila mtu kuwajibika kwa 24-7 yote, wanaweza kuchukua zamu ya saa moja au mbili kwa siku.
- Chukua 24-7 yako kwenye kituo cha karibu cha polisi – halafu unaweza kukuta kwamba hakuna matatizo tena ya usalama katika eneo lako. Utapata uzoefu wa matatizo ya jumuiya ile kwanza, na utaweza kuombea hali jinsi zinavyojitokeza.
- Jamii ya watu wenye hali moja (kikundi cha wachungaji) kinaweza kuonyesha kujitoa kwa kujifunga kwa umoja kwa jumuiya na Ufalme kwa kuingia kwenye 24-7, pamoja na wake zao.
- Anzisha 24-7 kupitia barua pepe.
- Tia moyo wafanyabiashara wa kiume na kike kushiriki katika 24-7 ili kwamba waweze kuiombea sekta ya biashara, kwa ajili ya shughuli za biashara za washindani wao wakubwa zaidi, na za mararikiri zao. (wanaweza kukabidhi biashara zao wenyewe kwa Bwana pia. Hebu fikiri nini kitakachotokea…).
- Uwe mbunifu. Huenda Bwana anapendezwa katika wazo lako. Usiogope mawazo ya ubunifu ambayo mwanzoni yanaweza kuonekana ya ajabu. Roho wa Bwana ni Roho wa ubunifu – Alikuumba wewe.
- Fikiria lindo la Neno. Kwa mfano chukua Biblia na uombe kutoka kwenye hiyo kwa wiki moja, usiku-na-mchana. Anza na Mwanzo 1, omba kiasi cha pale utakapofikia na kisha uanzie mwanzo tena. Uwezekano mwingine ni kuchukua Zaburi na kuomba kutoka hizo kwa siku saba. Unaweza pia kutoa sehemu ya ahadi, amri, na maombi katika Agano Jipya na kuomba kwa juma zima (sehemu kama hizo zinapatikana kutoka katika kuta za Yeriko info@iwipn.com; www.jwipn.com)

4:4 Mfano wa chumba cha maombi cha kuingiliana pamoja na vituo vya maombi.

Vituo vya maombi katika chumba cha maombi cha kuingiliana ni lazima, kwa kadri inavyowezekana, kumaliza aina zote za maombi, kama vile matakwa binafsi, maombezi, kutafakari, kunuia, kuabudu, kushukuru na kuungama. Mahali pazuri pa kuanzia ni ungamo binafsi, utakaso, msamaha na kujitoa kwa kujifunga binafsi ili kuenenda kulingana na njia za Mungu.

Ikijumuishwa katika sehemu hii ni "vituo vya maombi" 13, ambayo humaanisha maeneo 13 ambayo unaweza kupamba na kuweka samani ili kusaidia watu kuhusika zaidi kiutendaji katika maombi wanapoingia katika chumba cha maombi. Vituo hivi 13 vya maombi ni mifano michache tu ya kile kinachoweza kufanyika. Uwezekano wa aina na idadi ya vituo vya maombi na jinsi ya kupamba na kutumia chumba cha maombi ni karibu na kutokuwa na kikomo. Majina ya vituo vya maombi vinaweza kubadilishwa, vinaweza kuongozwa zaidi, baadhi vinaweza kuondolewa. Zaidi inategemea lengo la chumba cha maombi, ukubwa wa chumba, vitu vinavyopatikana kuweka samani/kupamba chumba hicho, umri wa watu watakaotumia chumba hicho cha maombi n.k.

A. Kuukabili Msalaba:
   - Muda wa kujichunguza, kumwomba Bwana afunue dhambi yoyote ambayo inazuia mwenendo wa kina naye. Kisha ipigilie msalabani.
   - Maandiko: Kol 2: 13, 14; Rum 6: 6; Gal 2: 20; 5: 24; Mt 16: 24; Isa 1: 18.
   - Vinavyohitajika: Msalaba (uliotengenezwa na vipande 2 bapa vya mbao), nyundo, misumari, vipande vya karatasi za rangi, kalamu, nguo nyekundu ambayo juu yake msalaba unalazwa juu ya sakafu, taa 1 ndogo ya pembeni mwa kitanda.

B. Mwenendo Uliofichika/Mwenendo wa Kina
   - Akisi juu ya uhusiano wako na Bwana na jitoe kwa kujifunga kujiweka wakfu upya kwa Bwana.
   - Maandiko: Rum 12: 1, 2; 2Kor 3: 18
   - Vinavyohitajika: Nguo nyeupe ya kupamba eneo hilo (ikiashiria matendo ya haki ya watakatifu), karatasi ya A4, karatasi, viti, mito, taa kubwa zenye mwanga mkali kwa ajili ya kumulika nyuma.

C. Mwenendo wa kukumbuka/Ukuta wa Ukumbusho:
   - Hii inaweza ama kuwa madhabahu ya Bwana, ambapo utaweza kuandika ahadi alizotoa Mungu na kuzitimiza, juu ya jiwe jeupe na uliongezea juu ya lundo la mawe kama madhabahu ya kutoa shukrani. Au inaweza kuwa ukuta wa matofali ambapo watu wanaweza kuandika ahadi alizotoa Mungu na kuzitimiza na kisha kumshukuru kwa kujenga ukuta.
   - Maandiko: Yos 4:21 0 24; Zab 26: 7; Flp 4: 6-7; Eze 22: 30; Isa 62: 6; 2Kor 1: 20.
   - Vinavyohitajika: mawe madogo (50), kalamu ziwekazo alama za kudumu, plastiki nyeusi, matofali 30 au karatasi kubwa za kuchora matofali juu ya ukuta, taa kubwa zenye mwanga mkali juu ya ukuta au taa za kusimamisha kwenye madhabahu.

D. Nyumba ya Mfinyanzi:
    - Mahali ambapo watu wanaweza kuja na kufanyiza chombo au pambo – kutafakari juu ya kazi ya Mungu katika maisha yao.
    - Maandiko*:* Isa 64: 8; Rum 9: 21
    - Vinavyohitajika: meza (iliyofunikwa na plastiki au gazeti), udongo wa mfinyanzi, viti, taa ndogo 1 ya pembeni mwa kitanda.

E. Kula pamoja Nami
    - Meza ya ushirika
    - Maandiko: Ufu 3: 20; Yn 6: 53-55; Mt 26-28
    - Vinavyohitajika: meza, vitambaa vya meza, vikombe, sahani, maji ya matunda, mkate, viti, vitaa vidogo vidogo vya rangi juu ya meza, mishumaa 2, viberiti/taa ndogo.

    Sehemu muhimu inayofuata katika chumba cha maombi inapaswa kuwa lango la nje kuelekea jumuiya yao na ulimwengu uliobakia.

F. Bakuli la Dhahabu/Ukuta wa Kuomboleza/Madhabahu ya Uvumba
    - Mahali ambapo watu wanaweza kuleta matakwa ya maombi mbele za Bwana kuhusiana na waliopotea, au hitaji lingine lolote walilo nalo katika maisha yao. Fanya hapa pawe mahali pa kupendeza kwa kuweka vipande vya karatasi juu ya kipande cha waya wa kuku au kutundika juu ya kamba ukitumia vibanuo vya nguo. Mulika eneo hili na taa mbili ndogo zenye mwanga mkali kutoka juu ya waya.
    - Maandiko: Mt 7: 7; Mt 21: 22; Yn 14: 13-14; 1Yoh 5: 15; Ufu 5: 8; 8:3-4
    - Vinavyohitajika: waya, ugwe wa kamba, vipande vya karatasi ya rangi, kalamu, bakuli la dhahabu, vibanio vya nguo, taa 2 ndogo zenye mwanga mkali

G. Ukuta wa Uhalisi:
    - Omba kwa ajili ya mahitaji ya jumuiya na ulimwengu
    - Maandiko: Mt 18: 19; Flp 4: 19
    - Vinavyohitajika: makala zilizokutwa kutoka za magazeti, vitu vya kugundishia ukutani, taa 2 ndogo zenye mwanga mkali kutoka juu.

H. Kuvunja ngome
    - Jenga gereza dogo. Weka meza ndogo ndani pamoja na kalamu, pipa la takataka, mshumaa, viberiti, beseni na jagi, taulo. Watu wanapaswa kuandika kwenye vipande vya karatasi, vile vifungo kwenye jamii zao zinazozuia maarifa ya Mungu, k.m. pombe, kutawaliwa na ngono, picha za uchi, ibada ya sanamu, umwagaji

damu n.k. kisha choma karatasi hiyo na uitupe kwenye pipa la takataka.

- Maandiko: Yn 8: 32; Yn 8: 36; Isa 61: 1
- Vinavyohitajika: Vigawanyi 3 vya chumba, nguo nyeusi, vipande vyembamba 14 vya mbao au mianzi ya kutengenezea madirisha 2 ya gereza, meza ndogo, karatasi, kalamu, mapipa ya takataka, mshumaa, viberiti.

I. Wavuvi wa Watu:

- Maombi kwa ajiii ya mataifa ya ulimwengu, taifa lako mwenyewe. Tumia ngano kuashiria kupanda Neno katika taifa hilo.
- Maandiko: Zab 2: 8; Mwa 24: 16; Kum 1: 21; Dan 7: 18; Mt 24: 14
- Vinavyohitajika: vigawanyi 2 vya chumba, ramani ya ulimwengu, ramani ya taifa lako, wavu wa kuvulia samaki, punje za ngano, vitu vya kugundishia juu ya ramani, taa yenye mwanga mkali kutoka juu ili kumulika zile ramani.

J. Miguu mizuri:

- Mahali ambapo watu wanaweza kutawadhana miguu, kuombeana, upatanisho
- Maandiko: Yn 13:5, 14, 2Kor 5: 18; Mt 5: 24
- Vinavyohitajika: Viti 6, beseni 3, ndoo 3, jagi 3, taulo 6, taa 1 ya kusimamisha

Sehemu muhimu ya mwisho katika chumba cha maombi lazima iwe sehemu chache za kukaza fikra juu ya Mungu, Ufalme wake na utukufu wake. Mahali kwa ajili ya kuabudu.

K. Mahali pa Siri/Chumba cha Kiti cha Enzi

- Mahali pa kukaa na kuakisi juu ya tabia ya Mungu, Majina yake. Kumwabudu eye kwa vile alivyo.
- Maandiko*:* Zab 95: 6; Wim 2: 10; Isa 55:1; Ufu 4:1; Mt. 5: 24
- Vinavyohitajika: Nguo za rangi za zambarau, nyeupe, dhahabu, Majina ya Mungu yakiandikwa juu ya kadibodi, viti/mito, chemchemi ya maji iliyojengwa kwa kutumia bomba, mimea, taa yenye mwanga mkali kutoka nyumba ya nguo, na moja kutoka chini ikimulika majina yale ya Mungu.

L. Lindo la Neno:

- Mahali ambapo watu wanaweza kukaa na kusoma Neno au Zaburi na kuakisi na kutafakari juu ya kile walichokuwa wakisoma.
- Vinavyohitajika: Meza ndogo, viti, taa 1 ya pembeni mwa kitanda, Biblia chache.

Ukuta wa Ubunifu:

- Mahali ambapo watu wanaweza kuandika, kuchora au kuchora picha za rangi za grafiti ukutani
- Vitu vinavyohitajika: meza (iliyofunikwa na plastiki au gazeti), rangi, vipande vya karatasi, pini, kalamu za rangi, penseli za rangi.

"Na Mungu je! Hatawapatia haki (kurekebisha kile kisicho sahihi) kwa wateule wake wanaomlilia usiku na mchana? Je atawangojesha kwa muda gani?" (Lk 18: 7-8).

Sio umri, uzoefu, kipaji au fedha zitakazodokeza hatima ya mataifa – maombi pekee yatabadilisha ulimwengu – Dick Eastman.

Katika kazi zote zinazoagizwa na Ukristo hakuna moja iliyo ya muhimu zaidi na bado inayopuuziwa zaidi kama maombi – Francois Fenelon.

SEHEMU YA 5

Nini cha kuombea:

5:1 Baadhi ya miongozo ya jumla juu ya nini cha kuombea

5:2 Viashiria vya maombi vya kutumia ili kuombea jumuiya, mji/jiji, nchi na ulimwengu wako.

Lindo za maombi zinaanzishwa kwa sababu mbalimbali na malengo mbalimbali. Baadhi yatalenga juu ya kanisa, baadhi juu ya majiji au jumuiya, na zingine juu ya idadi ya watu na/au mataifa ya ulimwengu. Yalengeshe maombi juu ya mahitaji ya ujumla katika maeneo yafuatayo:-

- Ulimwengu na bara lako mwenyewe
- Nchi yako
- Kila jiji/mji/mkoa
- Kanisa lako
- Familia yako
- Wewe mwenyewe

5:1 Baadhi ya miongozo ya jumla juu ya nini cha kuombea:

- Tumia Maandiko: ahadi kutoka katika Maandiko, Zaburi, maombi ya mitume katika AganoJipya, n.k.
- Tumia gazeti lolote la kila siku na ombea masuala yaliyoarifiwa katika gazeti lile.
- Jiandikishe kwa taarifa ya maombi ya barua pepe au nyaraka za maombi kutoka kwenye makanisa au mashirika ya Kikristo ambayo yanatuma taarifa (k.m. Kuta za Yeriko: www.jwipn.com).

- Katika miji/majiji/mikoa ambako kuna lindo za maombi za 24-7, taarifa rasmi za habari za maombi ya jumuiya zingeweza kutumwa kwa makanisa yote yanayoshiriki ili waombajii waweze kuomba kwa mapatano kwa ajili ya jumuiya zao.
- Mtu mmoja mmoja lazima ajisikie huru kuombea mahitaji yake binafsi pia.
- Kila mtu mmoja, mmoja ambaye anahusika katika lindo la maombi anaweza kutiwa moyo kuwaombea majirani wachache; wanafamilia au wenzi ambao bado hawajatoa mioyo yao kwa Bwana.
- Tenga muda wa kutosha kwa ajili ya kusifu na kuabudu. Tumia kuimba, kaseti/CD za muziki. Imba kwa utukufu wa Mungu; jifunze kumsifu na kumwabudu yeye. Zaburi zinafaa mahususi kwa ajili hii.

5:2 Viashiria vya maombi vya kutumia ili kuombea jumuiya, mji/jiji, nchi na ulimwengu wako.

1. Kuutafuta Ufalme wa Mungu – Kwa ajili ya nguvu ya mageuzi ya Ufalme wa Kristo.

   Kuhusiana na: giza la kiroho, faraka za kanisa, ukandamizaji wa kiuchumi.

   Mdo 1: 3-4 "….. *na kuyanena mambo yaliyouhusu ufalme wa Mungu. Akiwakusanya pamoja, aliwaagiza wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba, "ambayo" alisema, "mlisikia habari zake kwangu…".* Kwa ajili ya utukufu wa Kristo.

   - Kwa ajili ya mioyo ya watu wa Mungu kuwaka kwa upendo na utii aminifu kwa Yesu kama Mfalme na Bwana wa wote.
   - Kwa ajili ya wema na utukufu wa upendo wa kifalme wa Kristo kupatikana na wengi kotekote katika majiji yote
   - Kwa ajili ya Kristo kuwakusanya na kuwafundisha watu wake kuhusiana na tumaini la ufalme wake utoao uzima
   - Kwa ajili ya baraka za mataifa
   - Kwa ajili ya Kristo kuwaweka waumini katika miji ambapo upenyo wa baraka bado haujatokea. Omba kwamba watazifuatilia kwa uvumilivu ahadi ya Mungu ya baraka ya ufalme wake katika sehemu hizo ngumu.
   - Kwamba nguvu ya upendo wa Kristo utaleta mageuzi ya kudumu kotekote katika jumuiya zote.

2. Kuongezeka katika maombi ya pamoja – kwa ajili ya wendo endelevu wa maombi ya pamoja.

Kuhusiana na: kutokuwa na maombi, vitendo vya mizungu, tamaa ya vitu.

Mdo 1: 14 – *"Hawa wote walikuwa wakidumu kwa moyo mmoja katika kusali…?"*

Kwa ajili ya utukufu wa Kristo

- Kwamba Mungu angetulinganisha katika maombi kwa "moyo mmoja", (Mdo 1: 14; 2: 46; 4: 24), akitutia nguvu ili kuomba pamoja kwa shauku kwa ajili ya utukufu wa Kristo katika ulimwengu wote.
- Kwamba Mungu angesikia na kujibu maombi ya maskini, wachanga na wasiojiweza na atukuzwe kwa sifa zao.

Kwa ajili ya baraka za mataifa:

- Kwamba Roho wa Mungu angewachochea na kuwatia nguvu waumini ili kuomba baraka mahususi juu ya majirani na marafiki zao.
- Kwamba watu kotekote katika jumuiya zetu wangesukumwa kumlilia Mungu kwa msaada wake kwa jinsi ambavyo haijawahi kutokea.
- Kwamba viongozi wa jumuiya yetu wangemwomba Mungu kwa ajili ya hekima na tumaini lake.

3. Kujazwa na Roho Mtakatifu – kwa ajili ya Mungu kumwagia roho yake juu ya wote.

Kuhusiana na: kiburi cha usomi, ukandamizaji wa kipepo, upofu wa kiroho.

Mdo 2: 17 *"Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu…"*

Kwa ajili ya utukufu wa Kristo

- Kwa ajili ya Kanisa kujazwa upya na Roho ya Mungu, kutiwa nguvu kama watumishi wa Kristo wanaoshuhudia ulimwenguni
- Kwa ajili ya Roho wa Mungu kumfunua Yesu kwa wale waliozikwa katika giza la kiroho

Kwa ajili ya baraka za mataifa

- Kwamba Mungu angemwaga Roho yake juu ya kila mtu aliye hai ulimwenguni

- Kwamba Roho wa Mungu angewaamsha mataifa wasikie sauti yake na kuona kazi zake (Mdo 2:33)
- Kwa ajili ya wengi kuchochewa na ndoto zitolewazo na Roho ili kuona maono ya Yesu aliye hai na akitenda kazi katika maisha yao.

4. Kumgeukia Mungu katika toba – kwa ajili ya wengi kugeuka kutoka dhambini kwenda kwenye maisha mapya katika Kristo.

   Kuhusiana na: picha za ngono, mazoea ya tabia mbaya, uasi, ufisadi.

   Mdo 3: 19 – "*Tubuni basi, mrejee kwa Mungu, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana".*

   Kwa ajili ya utukufu wa Kristo
   - Kwa ajili ya Kristo kukutana na watu na upendo wake unaosamehe, ili mamilioni wageuke kutoka kwenye dhambi zao kwenda kwenye furaha ya kumfuata yeye.
   - Kwamba Roho wa Mungu angewasaidia watu kutambua jinsi walivyomhuzunisha Mungu na kuungama dhambi zao kwa uwazi.
   - Kwamba neno la msalaba wa Kristo lingevunja uwezo wa nguvu ya dhambi. Kwamba wengi wangesukumwa na tumaini kwa ajili ya dhambi zao "kufutwa" (Mdo 3: 19)

   Kwa ajili ya baraka za mataifa
   - Kwamba Mungu angewabariki watu wake kwa kuwasaidia kuwa wa kwanza kugeuka "kutoka kwenye njia zao mbaya" (Mdo 3: 26) ili nyendo imara za toba zikumbe jumuiya zote kijumla.
   - Nyendo za toba zingeleta "nyakati za kuburudishwa" (Mdo 3: 19) ili wanaume, wanawake na watoto wapate uzoefu wa uwepo wa Mungu.

5. Kuiandama amani ya Kristo – Kwa ajili ya mahusiano kugeuzwa. Kuhusiana na: ubaguzi wa kimbari, umaskini, vurugu, uhalifu.

   Mdo 2: 43 – 47 *"Kila mtu akaingiwa na hofu … wote walioamini walikuwa mahali pamoja … wakiuza mali zao na vitu vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja … wakimega mkate katika nyumba zao na kula pamoja kwa furaha na kwa mioyo mieupe, wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote…".*

Kwa ajili ya utukufu wa Kristo:

- Kwamba Mungu angeleta upenyo wa amani ya Kristo ulimwenguni kote kupitia maisha yaliyobadilishwa ya watu wake.
- Kwamba upatanisho kati ya makanisa ungeondoa faraka na uhasama, kuonyesha mahusiano kati ya Wakristo kwa upendo, furaha na ukunjufu wa moyo
- Kwa ajili ya Kristo kutembea kwa nguvu sana na kwa dhahiri ili watu wake pamoja na ulimwengu unaotazama "ujazwe na hofu" (Mdo 2: 43).

Baraka za Mataifa:

- Kwa ajili ya watu wa Mungu kugeuka kutoka kwenye ulafi na tamaa za dunia na kuwa wakarimu zaidi jinsi ambavyo haijawahi kutokea kabla.
- Kwa ajili ya Mungu kuingilia kati katika vita, akizuia nguvu za kiroho za uovu, akitiisha ugaidi, na kulinda maisha ya wale walioumizwa.
- Kwa ajili ya Mungu kuwatumia Wakristo kusaidia kuinua watu kutoka kwenye ukandamizaji wa umaskini uliokithiri. Inakisiwa kwamba zaidi ya watu bilioni wanapambana kuendelea kuishi kwa chini ya dola moja kwa siku.

6. Kutia nguvu kizazi kijacho – Kwa ajili ya kusudi la Mungu kwa famila na watoto.

Kuhusiana na: nyumba zilizovunjika, upotovu wa ngono, kazi za watoto, kutoa mimba Mdo 2: 39 – *"kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na watoto wenu…"*

Kwa ajili ya utukufu wa Kristo

- Kwa ajili ya Kristo kuimarisha ndoa na nyumba
- Kwa ajili ya vijana kumfuata Kristo mapema katika maisha, wakimtumikia kwa maisha ya moyo mkuu wa ibada
- Kwamba viongozi vijana wangetambuliwa na kuachiliwa ili kusaidia makanisa kukua kwa njia za kujizidisha (Mdo 6: 37)

Kwa ajili ya baraka za mataifa:

- Kwamba Wakristo wangeonyesha kwa ujasiri upendo wa huruma wa familia ya Mungu kwa yatima, wajane na wasio na makazi
- Kwa ajili ya Mungu kutumia watu wake kueneza upendo wake wa ubaba kwa mamilioni ya watoto walioachwa yatima na vita na ugonjwa wa mlipuko wa VVU/UKIMWI

- Kwa ajili ya Mungu kutia nguvu kizazi kijacho ili kitimize ahadi zake kotekote duniani.

7. Kuvumisha wito wa Mungu – Kwa ajili ya mataifa kusikia sauti ya Mungu.

   Kuhusiana na: ibada ya sanamu, kutokuamini, majonzi, kutokujua kusoma na kuandika.

   Mdo 2: 39 – *"… na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjue".*

   Kwa ajili ya utukufu wa Kristo
   - Kwa ajili ya Neno la Mungu kutangazwa kwa watu wa kila lugha, kabila na taifa (Mdo 1:8)
   - Kwamba ulimwengu ungesikia juu ya "matendo makuu ya Mungu" katika maneno ya lugha yao wenyewe na njia ya utamaduni wao wenyewe (Mdo 2: 11)
   - Kwa ajili ya Kristo kufuatwa miongoni mwa maelfu ya vikundi vya watu wasiofikiwa ambao wanakosa makanisa muhimu yanayokuwa na kujizidisha.

   Kwa ajili ya baraka za mataifa;
   - Kwa ajili ya Biblia kutafsiriwa kwa vikundi 3000 vya watu wasio na hata mstari mmoja katika lugha yao.
   - Kwamba Mungu angewaita wengi kwake (Mdo 2: 39) ambao wangemwita ili waokolewe (Mdo 2: 21)

8. Kuteseka pamoja na nguvu kwa ajili ya utukufu wa Yesu – kwa ajili ya ujasiri wa uaminifu kwa watu wake.

   Kuhusiana na: mateso, udhalimu, ugaidi Mdo 5: 41 – *"… wakifurahi kwa sababu wamehesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya Jina hilo".*

   Kwa ajili ya utukufu wa Kristo:
   - Kwamba wale ambao wanapingwa kwa sababu wanamtumikia Kristo wataonyesha tabia ya Yesu ya upole, ujasiri *(*Mdo 4: 13).
   - Kwa ajili ya Wakristo ambao wanateseka kwa ajili ya jina la Kristo ili kuwa thabiti katika furaha na imani
   - Kwa ajili ya Mungu kutukuzwa kwa matendo yake makuu katika sehemu ambazo amekuwa akipingwa (Mdo 4: 21)

Kwa ajili ya baraka za mataifa:

- Kwa ajili ya viongozi na serikali zetu kubarikiwa
- Kwamba viongozi wa serikali wanaompinga Kristo (Mdo 4: 25 – 27) wangebarikiwa na hekima ili kwamba wasije wakaonekana kuwa "wanapigana na Mungu" (Mdo 5: 39).

9. Kuleta uponyaji wa Kristo – Kwa ajili ya Kristo kuleta uponyaji maridhawa.

Kuhusiana na: ukosefu wa utunzaji wa kiafya, ugonjwa wa mlipuko wa UKIMWI, uchawi, uchafuzi wa mazingira Mdo 4: 30 – "*Ukinyosha mkono wako kuponya; ishara na maajabu vifanyike kwa jina la Mtumishi wako mtakatifu Yesu".*

Kwa ajili ya utukufu wa Kristo:

- Kwamba jumuiya zingeona mkono wa Kristo, ukinyoshwa, kuleta uponyaji wa kimiujiza miongoni mwa wagonjwa (Mdo 5: 14 – 16)
- Kwamba Jina la Yesu litangazwe kwa ishara na maajabu katika uwepo wa wengi (Mdo 3: 16)

Kwa ajili ya baraka za mataifa:

- Kwa ajili ya mwisho wa VVI/UKIMWI katika kizazi chetu
- Kwa ajili ya Wakristo kutenda kwa hekima na huruma endelevu ili kukomesha magonjwa
- Kwa ajili ya Wakristo kujishughulisha na kutoa utunzaji wa kiafya wa msingi mahali ambapo uhitaji ni mkubwa. Maelfu ya watoto wanakufa kila siku ulimwenguni kote kutokana na magonjwa yanayozuilika.
- Kwa ajili ya Mungu kutenda kazi kwa nguvu hapo watu wake wanapotenda kazi kwa busara ili kuleta uponyaji katika nchi.

10. Kueneza baraka za Kristo - Kwa ajili ya baraka iliyoahidiwa miongoni mwa watu wote.

Kuhusiana na: njaa, vita, makundi ya wahuni, rushwa Mdo 3: 25 – *"Alimwambia Ibrahimu, "katika uzao wako watu wa duniani watabarikiwa*".

Kwa ajili ya utukufu wa Kristo

- Kwa ajili ya Wakristo kuishi katika matazamio kwamba ahadi ya kale ingetimizwa hatimaye, ikileta mageuzi kwa jumuiya na nchi zao.

- Kwamba Yesu, mzao mkuu wa Ibrahimu, angeonekana kwa wote kwamba yuko miongoni mwa watu wote
- Kwa ajili ya makanisa kutenda kazi pamoja katika jina la Yesu kama familia moja, yakitenda kazi pamoja na Mungu kubadilisha maisha, majiji na mataifa

Kwa ajili ya baraka za mataifa

- Kwa ajili ya uadilifu na haki ya Mungu kugeuza njia za biashara na siasa, ikisafisha jamii nzima kutoka kwenye laana ya rushwa
- Kwa ajili ya amani ya ufalme wa Kristo kubadilisha njia ambazo miji na mataifa yanavyotawaliwa
- Kwa ajili ya furaha ya ufalme wa Kristo kulipuka katika sherehe za sifa za kushukuru miongoni mwa kila kikundi cha watu duniani

Na sheria (Neno) yake huitafakari mchana na usiku (Zab 1: 2)

Maombi si kwa zaidi sana kutenda kama yalivyo mwelekeo wa kumtegemea Mungu – Arthur Pink

SEHEMU YA 6

Jinsi ya kutmia saa moja katika maombi:
Muhtasari wa maombi ya saa moja

6:1 Kielelezo 1: Tafuta uso wangu
6:2 Kielelezo 2: Saa inayoubadilisha ulimwengu

Iliyojumuishwa ni miongozo miwili ya vielelezo vya maombi juu ya jinsi ya kuijaza saa na maombi. Vielelezo hivyo vyote viwili vinafanya kazi juu ya msingi wa kuchukua saa moja na kuigawanya katika nafasi 12 x dakika 5. Kwa kuiombea kila sehemu kwa dakika 5 utajaza saa na maombi.

6:1 Kielelezo 1 (Mwongozo wa Kivitendo juu ya jinsi ya kuomba kwa saa moja)

1. Nitafuteni Uso Wangu kupitia kuliitia Jina Langu (dk 5)
Yahwe chimbuko la saburi na faraja yote (Rum 15:5). Mungu mwenye huruma na rehema (Kut 34: 6), El-Shaddai (Mwenyenzi, Mwenye kujitosheleza, Mtoshelezaji (Mwa 12: *1)* Yahwe Ropheka (Bwana akuponyaye (Kut 15: 26), Yahwe Shalom (Bwana anatoa raha; Bwana ni amani (Zab 35: 27), Mfalme wa dunia yote (Mik 4: 13), Yesu Kristo Njia, Kweli na Uzima (Yn 14: 6*),* Kristo Nguvu na Hekima ya Mungu (1Kor 1: 24), Mwana-Kondoo aliye katikati ya kiti cha enzi (Ufu 7: 17), Mwana kondoo aliyechinjwa (Ufu 5: 12*)* Kristo

Tumaini la utukufu *(Kol 1: 27),* Roho ya Uhuru, Umaizi, Ushauri, Nguvu, Maarifa na Kumcha Bwana *(Isa 11: 2),* Neema na Maombi, Utakatifu, Upendo, Kweli, Nguvu, Kiasi, Hekima na Ufunuo wa Maarifa yake, Roho ya Utukufu.

2. Nitafuteni Uso wangu kwa ajili ya uamsho binafsi (dk 5)
   Jiulize maswali yafuatayo:-
   - Je! Kuna dhambi yoyote inayojulikana isiyoungamwa katika maisha yangu?
   - Je! Nina kutokusamehe au uchungu katika maisha yangu?
   - Je! Kuna vitendo au shughuli zenye kuonewa mashaka katika maisha yangu?
   - Je! Ninamtii Roho Mtakatifu mara katika mambo yote?
   - Je! Ninamkiri Yesu bila haya?

3. Nitafuteni Uso Wangu kwa ajili ya familia na marafiki zenu wasiookoka (dk 5).
   1.
   2.
   3.
   4.
   5.

   Ombea wokovu wao, kwamba Mungu atawabariki (kiroho, kijamii, kihisia) na kuombea mahitaji yao yanayowagusa.

4. Nitafuteni Uso Wangu kwa ajili ya kanisa (dk 5)

   Andika mambo 5 ya kuombea kanisa lako la mahali pamoja na/au kanisa kwa ujumla.

   1.
   2.
   3.
   4.
   5.

   na/au
   - Omba kwa ajili ya sharika kurejezwa kama nyumba za maombi kwa mataifa yote (Isa 56: 7, Mt 21: 13)
   - Omba kwa ajili ya sharika kutimiza Agizo Kuu (Mt 28: 18 – 20)

- Omba kwa ajili ya sharika kutimiza Amri Kuu (Mt 22: 37 – 40)
- Omba kwa ajili ya uamsho wa kiroho katika *kanisa (Efe 3: 17 – 23)*
- Omba kwa ajili ya kanisa kwamba liwe aminifu kwa Neno na lifae katika kushughulikia mahitaji ya watu *(2Tim 3: 1 – 17)*

5. Nitafuteni Uso Wangu kwa ajili ya mahitaji yenu binafsi (dk 5)

   1.

   2.

   3.

   4.

   5.

6. Nitafuteni Uso Wangu kwa kuomba kupitia Neno langu (dk 5) Anza kwa kuomba hatua kwa hatua kupitia Zaburi. Soma na kuomba kupitia Zaburi 2-3 kila wakati.

7. Nitafuteni Uso Wangu kwa kunisikiliza Mimi na kuningojea (dk 5). Kutafuta Uso Wake kwa kumtazamia na kumsikiliza. Soma Isa 42: 8-9, Dan 9:9-10; na Zaburi 25: 4-5. Mwombe Mungu akufunulie mambo mapya, mambo ambayo anataka uyaweke maanani na kuyazingatia. Mwombe akufunulie mapenzi na mikakati/mipango yake kwako. Mwombe kwa ajili ya mambo ambayo yako moyoni mwake ambayo anataka uyaombee. Uyaandike (jarida) kila unachohisi anakuambia.

8. Nitafuteni Uso Wangu kwa ajili ya baadhi ya masuala ya migogoro ulimwenguni kote.
   - Maradhi yalioenea pote ya VVU/UKIMWI
   - Rushwa katika ngazi zote
   - Kanisa linaloteswa katika nchi nyingi
   - Vita, umwagaji damu, vurugu za kikabila – pia omba kwa ajili ya mamilioni ya wakimbizi
   - Watoto katika dhiki: udhalilishaji na unyonyaji

9. Utafuteni Uso Wangu kwa ajili ya mataifa (dk 5))
   Andika majina ya nchi tano na uziombee

   1.

   2.

   3.

4.

5.

- Kwa ajili ya uamsho
- Kwa ajili ya wokovu wa wasiofikiwa na wasiookoka
- Kwa ajili ya viongozi waliopevuka na wanaomcha Mungu
- Kwa ajili ya uzidisho wa wafuasi wa Yesu waliojiweka wakfu
- Kwa ajili ya kuamsha maono ya umisheni katika sharika za mahali pamoja

na/au

- Omba kwamba mataifa yataona kwamba Kristo Yesu ni Njia, Kweli na Uzima *(Yn 14:6)*
- Omba kwamba watu wa dunia wasiofikiwa watafikiwa na Injili (Lk 24: 46-48)
- Omba kwa ajili ya ujio wa amani na utukufu wa Mungu kwa nchi na mataifa (Zek 9: 10)
- Omba kwamba wafalme na serikali zitatii Ubwana wa Yesu kama Mfalme wa Wafalme (Isa 49:7)
- Omba kwamba Mungu atayabariki mataifa (Yer 4: 1-2)

10. Nitafuteni Uso Wangu kwa ajili ya mapenzi Yangu yatendeke duniani (dk 5)

- Kwa ajili ya ufunuo wa utukufu wa Mungu juu ya dunia yote
- Kwa ajili ya uponyaji wa mataifa
- Kwa ajili ya upatanisho katika ngazi zote (familia, makanisa, vikundi vya kikabila au mbari, nchi n.k.)
- Kwa ajili ya uvunjaji wa ngome, miundo na mifumo ya kisiasa ambayo inaharibu maisha ya watu
- Omba kwa ajili ya baraka ya Mungu juu ya mataifa

na/au

Nitafuteni Uso Wangu kwa ajili ya watu kupatanishwa Nami na kila mtu na mwingine (dk 5).

- Omba kwamba mataifa yataungama kama wamewatendea vibaya, kuwaumiza au kuwakandamiza watu wao wenyewe au mataifa mengine na kwamba watakomesha mwelekeo wao wa kujishusha hadhi.
- Omba kwa ajili ya upatanisho katika ngazi zote (katika familia, ukandamizaji wa wanawake na watoto, kati ya makanisa na madhehebu, vikundi vya kikabila au mbari, kati ya mataifa, n.k.)

- Omba kwa ajili ya ondoleo la ngome, miundo na mifumo ya kisiasa ambayo inaharibu maisha ya watu.

11. Nitafuteni Uso Wangu kwa ajili ya vijana:
    - Kwamba kizazi hiki cha vijana kitafikia kizazi chao wenyewe na Injili
    - Kwa ajili ya vijana kuja kwenye uhusiano mpya wa ndani na Mungu na utii kwake
    - Kwa ajili ya wanafunzi waliojitoa kabisa, wakiishi katika utakatifu
    - Kumtumikia Mungu kabisa na kumfuata po pote anapoongoza
    - Kwa ajili ya mioyo yenye huruma, ili kuwafikia hata maskini na wenye taabu sana na kuwatumikia

12. Nitafuteni Uso Wangu kwa kusifu na kuabudu
    Malizia muda wako wa maombi kwa sifa na kuabudu. Soma yo yote mojawapo ya Zaburi 144 – 150. Mshukuru Mungu kwa wema wake na chukua muda kubariki watu mmoja mmoja wanaokuja maanani, katika Jina la Bwana Yesu Kristo.

6:2 Kielelezo 2 (Mwongozo wa Kivitendo juu ya jinsi ya kuomba kwa saa moja).

Saa inayoubadilisha ulimwengu.

Katika kitabu chake saa inayoubadilisha ulimwengu, Dick Eastman anapendekeza kwamba unaigawanya saa moja katika vipindi 12 vya dakika tano. Baada ya kila dakika tano, unaendelea kwenye namna nyingine ya maombi.

1. Sifa na kuabudu ni kitendo cha kupenda sana na kujiweka wakfu kwa Mungu (dk 5).

   Zab. 115:1 *"Ee Bwana, kutukuza usitutukuze sisi, bali ulitukuze jina lako, kwa ajili ya upendo na uaminifu wako".*

   - Mwabudu Mungu kwa vile alivyo, Mmoja aliyekuumba kwa Neno lake lisiloshindwa; kwa wokovu wako; kwamba umejumuishwa katika mpango wake.

   - Ni kwa kumwinua na kumheshimu Mungu.

   - Ni kwa kumtambua Mungu kwa vile alivyo, kumwadhimisha kwa maneno, utu wetu wote na kwa nafasi yetu ya maombi.

- Lisifu Jina lake, haki, upendo, utakatifu, kuweza yote, ukuu, uaminifu, kujua yote, Neno lake, uumbaji wake, kazi yake ya ukombozi, n.k. Unaweza kuchagua hoja tofauti ya kutumia kila wakati katika muda huu wa sifa na kuabudu. Panua hoja hii kwa kadiri iwezekanavyo, itafakari, na fikiria nini itakuwa maana ya kivitendo kwa maisha yako na maisha ya watu wengine.

2. Umgojee Bwana katika tendo la kujisalimisha na upendo na ustahi kwa Mungu (Mara nyingi pasipo maneno) (dk 5).

   Zab. 46: 10: Acheni mjue ya kuwa Mimi ni Mungu.

- Hapa ndipo nakuwa kimya mbele za Mungu.

- Mahali ambapo ninafunga mlango katika roho kwa mvuto wo wote kutoka ulimwenguni.

- Mahali ambapo ninakuja kwenye uwepo wake kupitia tendo la imani.

- Hii ni kumsifu na kumwabudu Mungu kwa vile alivyo.

- Wakati wa kipindi hiki cha kimya, tunakaza juu ya Mungu na kujiweka wakfu tena kwa Mungu. Tunafurahi katika uwepo wake na juu ya uwepo wake.

- Huu ni wakati wa mawasiliano binafsi ya kina na undani na Mungu, hapa ndipo mimi, kama kiumbe mwenye kikomo na mipaka ninaingia katika uwepo wa Mungu, Asiye na mipaka na Asiye na kikomo.

- Kwenye hatua hii, inapaswa tuhakikishe kwamba tuna mawasiliano yaliyo hai na Mungu. Wakati huu wa muda wa kumngojea Bwana hakuna nafasi ya pupa na kuwa na haraka, hatuwezi kuharakishwa.

- Wakati wa kipindi hiki, hufikirii juu ya kitu kingine isipokuwa Mungu Baba, Mwana wake Yesu Mwokozi wako na Roho Mtakatifu.

- Huna haja ya kuweka mawazo yanayokuja kwenye maneno. Makinisha juu ya uhusiano wako na Mungu na upendo wako kwake.

3. Ungamo/fedheha ni tendo la kuungama na utakaso wangu kama hekalu la Mungu ili kunipa mlango huru kwenda kwa Mungu (dk 5) Hakika mkono wa Bwana si mfupi hata usiweze kuokoa, wala sikio lake si zito sana hata lisiweze kusikia; lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone,

hata hataki kusikia (Isa 59: 1 – 2). Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote (1Yoh 1: 9).

- Hapa ndipo ninapokiri dhambi zangu, kuungama hatia yangu, kukubali kwamba nimekosa, kugeuka mbali nayo na kuukubali msamaha wa Mungu.

- Ndipo ninapomwomba Mungu anionyeshe namna yoyote ya kiburi na ukosefu wa upendo na kuungama na kuachana nayo.

- Huu ni wakati wa kujichunguza na kumruhusu Roho Mtakatifu kufunua dhambi yo yote isiyoungamwa. Tunapokea tu msamaha na ukombozi kutoka dhambini kupitia damu ya Bwana Yesu na kifo chake cha upatanisho msalabani.

- Ninapoungama dhambi zangu si lazima niombe kwamba Mungu abadilishe hali yangu ya mambo, bali kwamba anisamehe na kunibadilisha.

4. Kuomba Maandiko ni kujulisha kiroho na kuomba kulingana na dondoo na ufunuo wa Mungu (dk 5)

    - Haya ni maombi yaliyorutubishwa na Neno: Neno ni kitabu chako cha mwongozo cha jinsi ya kuomba.

    - Hii ni kuomba kulingana na ahadi za Mungu. Ahadi za Mungu katika Neno zinachochea imai yetu.

    - Biblia kwa nafasi ya kwanza ni kitabu ambacho kinapaswa kuaminiwa. Katika kipindi hiki ninauliza: Bwana, ni ahadi zipi ambazo napaswa kujitwalia, ni amri zipi ambazo ninapaswa kuzitii, ni maonyo gani ambayo napaswa kuwa makini nayo?

    - Tunapaswa kumkumbusha Bwana mchana na usiku juu ya ahadi zake katika Neno lake. Unaposoma Biblia, unapaswa kumwomba Bwana jinsi ya kuitumia kwa maisha yako ya kila siku na katika muda wako wa maombi.

5. Kukesha ni muda wa uchunguzi wa kiroho, kukesha kiroho, kuzingatia kiroho masuala yanayohitaji maombi (dk 5).
   Dumuni sana katika kuomba mkikesha katika kuomba huku na shukrani (Kol 4: 2)

- Kukesha na kuwa macho na mashambulizi yanayoweza kutokea kutoka kwa Shetani. Omba na muulize Roho Mtakatifu kukuonyesha mipango, njia, ngome na mikakati ya yule Mwovu.

- Kutambua uongozi wowote kutoka kwa Bwana

- Kutambua ufunuo wowote wa Mungu

- Uliza umaizi, upambanuzi, hekima na kuelewa kile cha kulenga katika maombi na vipi viwe vipaumbele vyako.

- Kufahamu mapenzi ya Mungu, mahali ambapo anataka kukutumia leo.

- Kumuuliza Mungu ni nini kilichoko katika dondoo yake na kwenye moyo wake.

- Je kuna lolote katika magazeti, runinga (TV) au redio tunalopaswa kuliombea, mambo kama matatizo ya kiuchumi, vurugu za kisiasa na vita ambavyo Mungu anatutaka tuombe?

6. Maombezi ni kusimama mahali palipobomoka kwa ajili ya watu wengine, ili kumakinikia mahitaji na matakwa ya watu wengine (dk 5).

   Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, mombezi na shukrani zifanyike kwa ajili ya watu wote, kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya utulivu na amani katika utauwa wote na ustahivu *(1Tim 2: 1-2).*

   - Kuomba kwa ajili ya mpango wa Mungu kwa ajili ya maisha ya watu wengine.

   - Kusimama kati ya Mungu na watu wengine na kuyaombbea mahitaji yao – kuomba kwa ajili ya rehema na neema.

   - Hii ni nafasi ya kiroho mbele za Mungu – kubakia umesimama hadi umepata hakikisho kwamba Mungu akusikia na kwamba anakufungua kutoka kwenye kuliombea.

   - Hii ni njia ya Mungu kuwahusisha watoto wake katika mpango wake na ulimwengu.

- Unapofanya maombezi, unasimama upande wa Mungu na kufanya kazi naye kwa ajili ya wokovu au kwa faida ya mtu mwingine.

- Kupitia maombi, unaweza kuhusika katika vita vya kiroho dhidi ya nguvu za Uovu. Omba na kumuuliza Bwana kufunua kwako, kupitia kazi ya Roho Mtakatifu mahali ambapo nguvu hizi zinatenda kazi. Kwa msingi wa mamlaka yako katika Kristo, unapaswa kuzifunga nguvu za shetani katika Jina la Yesu na kuharibu ngome na hoja zao. Mpinge ibilisi na usimpe mahali pa usalama. Yesu alimshinda yule mwovu pale msalabani. Sisi kama waumini tunapaswa kutangaza ushindi huu kwenye kila eneo la maisha.

7. Maombi kwa ajili ya mahitaji binafsi

   Utupe leo riziki yetu (Mt 6: 11) Yabesi alimlilia Mungu wa Israeli, "Lau kwamba ungenibarikia kweli kweli, na kunizidishia hozi yangu, na mkono wako ungekuwa pamoja nami, nawe ungenilinda na uovu, ili usiwe kwa huzuni yangu" Naye Mungu akamjalia hayo aliyoyaomba (1Nya 4: 10) Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu (Flp 4: 6)

   - Kuomba kwa ajili "riziki" yangu

   - Kuchukua dhiki, migogoro, mahitaji na matakwa yangu mwenyewe kwa Mungu.

   - Kwa unyenyekevu na utegemezi mkamilifu, namwomba Mungu alete mahitaji yangu, nakuja kama mtumishi wa Mungu na mtoto wake.

   - Usitoe masharti

   - Njoo kwa imani na kutumaini – njoo kama rafiki wa Mungu

   - Uwe mahususi

   - Kama Wakristo, tunaweza kwa ujasiri kupeleka mahitaji yetu binafsi kwa Baba. Tunaweza kuomba kwa matazamio, hata juu ya mambo madogo sana.

   - Uwe macho kwa ajili ya matakwa ya binafsi.

8. Kushukuru ni wakati ambapo kuthamini kwangu kwa Mungu kwa ajili ya utunzaji na ulinzi wake na kwa vile alivyo. Shukuruni kwa kila jambo, maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu (1The 5: 18)

    - Fikiri juu ya siku na mshukuru Mungu kwa ajili ya utunzaji wake kwa ajili yako na wengine.

    - Mshukuru Mungu kwa ajili ya mambo mapya aliyoyafanya: kiroho, kimwili, kijamii.

    - Mshukuru kwa vile alivyo, karama zake, majibu ya maombi … baraka zake zote.

    - Uwe mahususi katika kushukuru kwako.

9. *Kuimba ni sifa na kuabudu kwa tuni.*
   Mfanyieni Bwana shangwe, dunia yote, Mtumikieni Bwana kwa furaha; njoni mbele zake kwa kuimba, Jueni kwamba Bwana ndiye Mungu, Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake; tu watu wake na kondoo wa malisho yake, Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru, nyuani mwake kwa kusifu, mshukuruni, lihimidini jina lake, Kwa kuwa Bwana ndiye mwema, rehema zake ni za milele, na uaminifu wake vizazi na vizazi (Zab 100).

    - Hili ni tendo la kumsifu na kumwabudu Mungu kwa nyimbo za kiroho.

    - Hii inaweza kuwa kilio cha vita dhidi ya nguvu za giza. Kuimba na vita vya kiroho (kushindana kwetu dhidi ya yule Mwovu) ni sehemu isiyotanguka ya wao kwa wao.

    - Tumia nyimbo zinazojulikana vema au imba nyimbo zako mpya. Unaweza kuanza kwa kutumia sehemu za maandiko yaliyotolewa kuwa nyimbo.

    - Hii ni kumtukuza, kumheshimu sana na kumwabudu Baba katika wimbo.

10. Kutafakari ni kufikiria au kuchunguza suala kwenye kiwango cha kina, ili kulitathmini kiroho.

Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki; wala hakusimama katika njia ya wakosaji; wala hakuketi barazani pa wenye mizaha. Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo; na sheria yake huitafakari mchana na usiku. Naye atakuwa kama mti uliopandwa kando kando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani lake halinyauki. Na kila alitendalo litafanikiwa (Zab 1: 1-3). Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako; bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa humo. Maana ndipo uakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana *(Yos 1: 8).*

- Tafakari juu ya asili na hali ya Mungu wa Utatu, uumbaji, matendo (kazi) na tabia yake.

- Chukua hoja mahususi kutoka katika Maandiko na tafakari juu yake (haki, upendo, kweli, nuru, amani, utakatifu n.k.).

- Chukua sehemu kutoka katika Maandiko na tafakari juu yake.

- Mfanye Mungu mwenyewe awe lengo la kutafakari kwako: maneno au matendo yake, Neno lake, tabia yake.

Kutafakari Kikristo ni kinyume na kutafakari kwa Mashariki. Kutafakari kwa Mashariki ni juu ya hali ya akili isiyoonyesha hisia na kufanya akili yako kuwa tupu. Kwa Mkristo kutafakari ni mchakato tendaji wa kutathmini, kuchunguza na kuwaza ambapo akili yako inahusika kikamilifu na ambapo inaruhusu Roho Mtakatifu na Maandiko kukuongoza. Kutafakari ni kuakisi katika njia ya nidhamu. Uwe macho kwamba Shetani haweki mawazo yake akilini mwako. Pia, chunga mawazo hasi wakati huu. Akisi juu ya lo lote lililo la kweli, la staha, la haki, safi, lenye kupendeza na lenye sifa njema. Unapotafakari juu ya sehemu mahususi ya Maandiko, unapaswa kujiuliza kile ambacho sehemu hiyo inasema kwako binafsi.

11. Kusikiliza ni kipindi ambacho unapokea maagizo kutoka kwa Mungu, ambapo unamwomba Mungu akufunulie mambo anayokutaka uyaangalie na kuyazingatia.

Usiseme maneno ya ujinga kwa kinywa chako, wala moyo wako usiwe na haraka kunena mbele za Mungu; kwa maana, Mungu yuko mbinguni, na wewe upo chini, kwa hiyo maneno yako na yawe machache (Mhu 5: 2).

- Lenga kusikiliza sauti ya ndani ya Roho Mtakatifu.

- Ambapo anauliza: Unataka nifanye nini? Mapenzi yako ni yapi leo?

- Tafuta uongozi kutoka kwenye Neno.

- Mwombe Mungu kwa makusudi akufunulie mapenzi, mipango na mikakati yake.

- Kumngojea Bwana ni juu ya kumpenda Mungu. Wakati wa kutafakari, tunataka kujifunza zaidi juu ya Mungu. Katika kipindi cha kusikiliza, tunataka kusikia kile |Mungu anachotaka kutuambia. Wakati wa kipindi hiki, ninauliza; Bwana, unataka nini kutoka kwangu, mapenzi yako ni yapi kwa ajili yangu?

- Unaweza pia kumuuliza maswali mahususi; huenda ni maswali magumu ambayo kwayo huna majibu. Uwe makini kwa Roho Mtakatifu.

- Uwe mwangalifu usiwe mwepesi katika kusema: "Bwana alisema nami hili na lile"

12. Kusifu ni kumwadhimisha Mungu, kumtukuza, kumwambia kwamba unajua ni Nani uliyekuwa ukimwomba na kumtumaini kwa maombi yako.

    Kwa kuwa ufalme ni wako na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina (Mt 6: 13).

    - Fanya Amina yako yenye nguvu mwishoni ili kuthibitisha kwamba unaamini Mungu amekusikia na atakujibu. Amina inamaanisha : hii ni kweli na hakika, hii itakuwa hivyo.

    - Hiki ni kitendo cha mwisho cha kiroho cha kumweka Mungu juu ya kiti cha enzi cha maisha yako.

    - Hapa ndipo unapokiri: Kwa kuwa ufalme ni wako na nguvu na utukufu hata milele. Amina.

      Ufalme wako na uje, mapenzi yako na yatimizwe (Mt 6: 10)

      Kuna machozi mengi yanayomwagwa juu ya maombi yaliyojibiwa kuliko juu ya yale yasiyojibiwa – Teresa wa Avila.

SEHEMU YA 7

Kuomba Neno
7:1 Kwa nini tunapaswa kuomba Neno
7:2 Jinsi ya kuomba Neno
7:3 Maombi 30 ya Neno

Hudson Taylor anasema: "sisi (wakristo) ni watu wasio wa dunia hii: tuliozaliwa mara ya pili kupitia uzazi usio wa kidunia, tukiendeshwa na nguvu isiyo ya dunia na kulishwa na chakula kisicho cha dunia, kufundishwa na Mwalimu asiye wa dunia kutoka katika Kitabu kisicho cha dunia". E.W. Kenyoni alisema: Kufunga na muda mrefu wa maombi hayajengi imani … kusoma vitabu juu ya imani na watu wa imani na matendo yao kunachochea moyoni shauku ya kina kwa ajili ya imani, lakini haijengi imani. Neno peke yake ndilo chimbuko la imani. Andrew Murray alisema: Neno kidogo pamoja na maombi kidogo ni kifo kwa maisha ya kiroho. Neno kwa wingi pamoja na maombi kidogo yanatoa maisha yasiyo na afya nzuri. Maombi kwa wingi pamoja na Neno kidogo yanatoa maisha zaidi, lakini pasipo uthabiti. Kipimo kamili cha Neno na maombi kila siku hutoa maisha yenye afya na yenye nguvu.

Imani huja kutokana na kusikia ujumbe, na ujumbe unasikiwa kupitia Neno (Rm 10: 17). Pasipo imani hatuwezi kuomba kwa sababu kuomba pasipo imani hakumpendezi Mungu (Ebr 11: 6). Mungu hulithibitisha Neno lake na ahadi zake kwa kiapo (Ebr 6: 16 – 17). Hawezi kutokuwa mwaminifu kwa Neno lake. Ahadi zile zilizoko katika Neno zinaoana na hali yake na tabia yake, ambazo kwazo kamwe hawezi kutokuwa mwaminifu.

7:1 *Kwa nini tunapaswa kuomba Neno?*

- Tunapoelewa mamlaka ya Neno na nafasi ya Neno katika maisha yetu, inafuatia kwamba tunapaswa kuomba Neno. Zifuatazo ni baadhi ya sababu kwanini tunapaswa kuomba Neno.

- Mungu hujulisha mapenzi yake katika Neno. Tunapoomba Neno tunaomba mapenzi ya Mungu na tunapoomba kulingana na mapenzi ya Mungu, Neno linasema maombi yetu yatajibiwa (1Yoh 5: 14 – 15).

- Vitabu vya kidunia vinatoa maarifa na unaizi, lakini ni wakati tu tunaposoma Neno ndipo unapokuja kwenye imani. Tunapoomba Neno, imani inaongezeka katika mioyo yetu (Rum 10: 17).

- Neno/Maandiko yanafunua vipaumbele vya Mungu. Tunapoomba kulingana na Neno tunajifunza kwamba vipaumbele hivi ni vipi na

kisha tutaweza kurekebisha maisha yetu kulingana na vipaumbele hivi.

- Neno lina mamlaka. Mungu Baba alipoumba ulimwengu alifanya hivyo kupitia Mwanawe, Neno. Neno linanena neno na kulikuwa na nuru na uzima na watu na sayari za juu, nyota, jua, mwezi. Tunapotangaza Neno, linakuwa tangazo katika ufalme wa kiroho – Neno bado lina nguvu ile ile. Tunapoliitia Neno lililo hai, lina nguvu ya kutoa uzima na kuumba upya.

- Neno linatufundisha juu ya Mungu – tabia yake, hali, nguvu, uwezo na sifa bainifu. Tunapomfahamu Mungu vema zaidi tunaweza kuomba kwa imani zaidi. Imani ina nguvu kwa kadir ya mtu unayemwamini.

7:2 ***Jinsi ya kuomba Neno***

Yoyote kati ya njia zifuatazo za kuomba Neno zinaweza kufanywa kibinafsi, kwa pamoja au katika chumba cha maombi cha 24/7.

- Soma Neno: Njia rahisi sana ya kuomba Neno la Mungu ni kulisoma hasa kwa sauti (kulitangaza, kulikiri, kulitangaza Neno), kuanzia Mwanzo na kuishia Ufunuo.

- Zaburi: Kanisa la mwanzo liliweka msisitizo mkubwa juu ya kuomba Zaburi. Zaburi zina aina zote mbalimbali za maombi, kama vile kuadhimisha, kuabudu, sifa, kujinyenyekesha mbele za Mungu, maombi ya kujinyenyekesha, maombezi, vita vya kiroho na unabii. Ni kupitia kuomba Zaburi (waliomba kwa sauti na magotini) ambapo Kanisa la kwanza lilipata imani ili kuwafikia jamii za kipagani kwa Injili ya ukombozi.

- Ahadi za Mungu: Neno la Mungu lina ahadi lukuki juu ya hali nyingi, hali ya mambo na masuala. Kusoma, kutafakari na utangazaji wa Maandiko haya huongeza imani, na kutusaidia kuelewa jinsi Mungu anavyotutaka tutende katika hali za namna mbalimbali. Inatusaidia kuomba na kufanya maombezi kwa hekima na maarifa kuliko kutoa kwenye taswira ya hofi na fadhaa.

- Mapenzi na amri za Mungu: Kwa kusoma Neno, tunagundua mapenzi, amri na maagizo kwa ajili ya kanisa lake ulimwenguni. Jenga maombi yako katika amri na maagizo haya kutoka katika Maandiko.

- Unabii: Neno la Mungu limejaa unabii ambao bado unahitaji kutimizwa; unabii unaotuhusu sisi wenyewe, familia zetu, mataifa yetu na makusudi ya Mungu katika nyakati za mwisho. Tunahitaji kuomba unabii huu kwa ajili ya kutimizwa.

- Mstari kwa mstari: Unaposoma Neno, badili kila mstari unaoingia moyoni, kwenye maombi binafsi kwa ajili ya kukua kiroho, uponyaji wa kimwili na kihisia na yenye kutoa uzima, kuliko kushughulikia matatizo au masuala ya kilimwengu. Liweke upya Neno la Mungu kwenye maombi na liombe Neno lake kwake.

- Taamuli: Soma Neno kimya au kwa sauti kwa lengo la kukutana na Mungu. Wakati ambapo, kwa imani, roho yako inahisi uwepo wake, ruhusu Roho Mtakatifu akuchukue kwenye kuakisi au taamuli ya kina juu ya Nafsi ya Mungu. Kawia tu katika uwepo wake. Wakati mwingine maombi haya pasipo maneno yanaweza kuwa na athari ya kina kwetu na ulimwengu wetu kuliko maombi mengi tunayoyaomba kutoka kwenye akili zetu.

7:3 ***Maombi 30 ya Neno***

1 – Bariki jumuiya yetu.
Baba, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, tunataka kuomba kwamba ubariki jumuiya yetu. Kwamba utawabariki na kuwalinda, kwamba utawaangazia nuru za uso wako na kuwafadhili, kwamba utawainulia uso wako na kuwapa amani (Hes 6: 23 – 27). Tunaomba hili kwa ajili ya majirani zetu, wenzi wetu kazini, kwa ajili ya polisi na watu magerezani, kwa ajili ya watoto shuleni, madaktari na wauguzi na wagonjwa mahospitalini, kwa ajili ya akina baba na akina mama katika jumuiya yetu na kwa ajili ya biashara, waalimu mashuleni, halmashauri ya majiji na wakuu wa serikali, wale wasio na makazi, wale wasio na kazi, wale wanaohusika katika namna zote za kutawaliwa na ubaya, wale walio fukara, rais wa taifa letu na washauri wake, mawaziri wa serikali na watumishi wao wote.

Atukuzwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo Yesu (Efe 1:3). Kama Yabesi alivyomlilia Mungu wa Israeli, tunakulilia kwa ajili ya jumuiya yetu: Lau kwamba utatubariki, kwamba mkono wako uwe juu yetu, na kwamba utatulinda na madhara ili kwamba tuwe huru na maumivu na kwamba hatutasababisha maumivu (1Nya 4: 10).

Mungu wa amani, na ututakase kabisa. Roho, nafsi na mwili yote ihifadhiwe bila lawama (1The 5: 23 = 24). Bwana unaweza kutulinda tusianguke na kutuwakilisha sote mbele ya uwepo wako wa utukufu bila mawaa na kwa furaha kuu (Yud 24 – 25).

Bwana Yesu, neema yako na iwe juu ya jumuiya yetu (1Kor 16: 24).

2 - Tunaliinua Jina Lako
Baba yetu wa mbinguni, Wewe Uliye juu na Uliyetukuka, Mungu Aliye Juu Sana, Ukaaye milele; Jina lako ni takatifu (Isa 57: 15). Jina lako na litukuzwe na liadhimishwe katika jumuiya yetu (Mt 6: 9). Umetuamuru tusilitaje bure Jina lako, wala kulinajisi au kulikufuru Jina lako (Kut 20: 7, Law 19: 12, 24: 16). Na bado Jina lako limenajisiwa kati ya mataifa na watu wengi wamelisahau Jina lako na wamenyoosha mikono yao kwa miungu mingine (Eze 35: 23; Zab 44: 20). Tunaungama kwamba tumeihalifu amri yako. Tunavyoomba sasa na kulikiri Jina lako, na kugeuka kutoka katika dhambi yetu, tafadhali sikia na kuturejeza (2Nya 6: 32, 33). Jina lako na litakaswe ili kwamba mataifa yote, hata maadui zako wajue kwamba Wewe ni Bwana na waliche Jina lako (Eze 36: 21, 23; Isa 64: 2; Zab 102: 15).

Ee Bwana Mungu, mabwana wengine zaidi ya wewe wametumiliki sisi na jumuiya yetu, lakini sasa tunaliitia Jina lako (Isa 26: 13). Shauku ya nafsi yengu ni kwa ajili ya kumbukumbu ya Jina lako katika jumuiya yetu (Isa 26: 8). Na tulikumbuke Jina lako usiku ee Bwana na kulitafakari (Zab 119: 55; Mal 3: 16). Unganisha mioyo yetu ili iliche Jina lako ili kwamba tuondokane na uthalimu na kulishika sana Jina lako na kutokukukana (Zab 86: 11; 2Tim 2: 19; Ufu 2: 13, 3:8). Jina lako ni la ajabu, kama marhamu iliyomiminwa, ngome imara na mahali salama pa kukaa (Amu 13: 18; Wim 1: 3; Mit 18: 10; Zab 61:3).

3 – Kwa ajili ya Neema na Rehema za Mungu
Baba wa rehema, uyaelekee maombi yetu na dua yetu kwa ajili ya rehema kwa jumuiya yetu (1Fal 8: 28). Kama macho ya watumwa yatazamapo mkono wa Bwana wao, kama macho ya mjakazi yatazamapo mkono wa bimkubwa wake, hivyo macho yetu yakutazama wewe, Bwana Mungu wetu hadi utakapotuonyesha rehema zako (Zab 123:2). Tunakielekea kiti chako cha enzi cha neema kwa ujasiri ili kwamba tupokee rehema na kupata neema ba nsaada wakati wa uhitaji (Ebr 4: 16; Zab 5: 7; 6: 9, 28: 2). Usituzuilie rehema zako ee Bwana; fadhili zako na kweli yako na

zituhifadhi daima (Zab 40: 11). Maana kama mbingu zilivyoinuka juu ya nchi, ndivyo zilivyo kuu rehema zako kwa wale wakuchao. Wewe ni mwema; Rehema zako ni tangu milele hata milele na hudumu kutoka kizazi hata kizazi kwa hao wanaokucha (Zab 103: 11, 17; 106: 1; Lk 1: 50). Wewe ni mwenye huruma na mwenye neema; si mwepesi wa hasira, mwingi wa upendo na uaminifu, akidumisha upendo kwa maelfu na kusamehe uovu, uasi na dhambi. Na bado kuwaadhibu wenye hatia na kamwe hamhesabii mtu mwovu kuwa hana hatia, mwenye kuwapatiliza watoto uovu wa baba zao hadi kizazi cha tatu na cha nne. Wewe ni mwema kwa watu wote na rehema zako ni juu ya kazi zako zote (Kut 34: 6 – 7; Zab 145: 9). Ni huruma zako kwamba hatuangamii kwa kuwa rehema zako hazikomi.

Ujapohuzunisha, unaonyesha rehema kwa kadiri ya wingi wa huruma zako (Omb 3: 22, 32). Katika ukuu wako ulitangaza "nitamfadhili yeye nitakayemfadhili, na nitamrehemu yeye nitakayemrehemu" (Kut 33: 19; Rum 9: 16, 18). Usizuilie rehema zako, ee Bwana, fadhili zako na kweli yako zituhifadhi daima (Zab 40: 11).

4 – Tunakuabudu

Utukufu una wewe milele (Rum 11: 36). Wewe u Mfalme milele, asiyeweza kuona uharibifu, asiyeonekana, Mungu peke yako, kwako iwe heshima na utukufu milele na milele (1Tim 1: 17). Tunakubariki, Mungu wetu, Mtawala pekee, Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, ambaye peke yake hapatikani na mauti, amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa wala hakuna mwanadamu aliyemwona wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una wewe hata milele (1Tim 6: 15 – 16).

Bwana, tunatangaza kwamba hapo mwanzo ulitia misingi ya dunia, na mbingu ni kazi za mikono yako. Hizo zitaharibika, bali wewe utadumu, nazo zote zitachakaa kama nguo. Na kama mavazi utazizinga nazo kama nguo zitabadilika. Lakini wewe yule na miaka yako haitakoma (Ebr 1: 10 – 12). Bwana Yesu, wewe ni mzaliwa wa kwanza kutoka kwa wafu, na mkuu wa wafalme wa dunia. Unatupenda na umetuweka huru kutoka dhambini kwa damu yako, na umetufanya kuwa ufalme na makuhani ili kukutumikia wewe na Mungu Baba yetu. Wewe ni Alfa na Omega, aliyeko, na aliyekuwako na atakayekuja, Mwenyezi (Ufu 1: 6 – 20). Umestahili, Bwana na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza, kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako navyo vikaumbwa (Ufu 4: 8 – 11). Astahili

Mwana-Kondoo, aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka! (Ufu 5: 8 – 14). Ni makuu na ya ajabu, matendo yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi, Ni za haki na za kweli, njia zako, Ee Mfalme wa mataifa. Ni nani asiyekucha, Ee Bwana, na kulitukuza jina lako? Kwa kuwa peke yako u Mtakatifu; kwa maana mataifa yote watakuja na kusujudu mbele zako, kwa kuwa matendo yako ya haki yamekwisha kufunuliwa (Ufu 15: 1 – 8).

5 – Kwa ajili ya neema na rehema zako.
Mungu mwenye rehema, ponya jumuiya yetu, hata ingawa tumekutenda dhambi na kiasi cha wingi wa rehema zako uyafute makosa yetu katika jumuiya hii (Zab 41: 4; 51: 1). Tunapoficha dhambi zetu, hatutafanikiwa, kwa hiyo tunaungama na kuziacha dhambi zetu ili kwamba tupate rehema kwako (Mt 28: 13). Usikumbuke juu yetu dhambi za baba zetu, rehema zako zije kutulaki hima, kwa maana tumedhilika sana (Zab 79: 8).

Ni nani aliye Mungu kama wewe, mwenye kusamehe dhambi na kuachilia makosa na hashiki hasira bali hufurahia kuonyesha rehema? (Mik 7: 18). Hurumia watu katika jumuiya yetu kama ulivyoirehemu Israeli. Usitukomeshe au kutuacha, kwa maana wewe u Mungu mwennye neema na mwenye rehema. Acha wale wasiopokea rehema, wapokee rehema zako sana, ili kwamba wakutukuze (Neh 9: 31; 1Pet 2: 10; Rum 15: 9).

Umetuonyesha yaliyo mema, kwa ajili yetu na kile unachotaka kutoka kwetu: Kutenda haki, kupenda rehema na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wetu (Mik 6: 18). Ututie nguvu ili tufanye mapenzi yako; utusaidie kufuata mfano wako ili kutoa haki ya kweli na kuonyesha rehema na huruma kila mtu kwa mwenzake. Heri wenye rehema, maana hao watapata rehema (Zek 7: 9; Mt 5: 7; Rum 12: 10). Tusiipuuze haki, rehema na uaminifu (Mt 23: 23). Pamoja na Kanisa katika zama zote tunalia: Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu Aliye Hai uturehemu (Mt. 9: 27; Lk 18: 38; Mt 15: 22). Ongeza rehema, amani, na upendo wako kwetu (Yud 2).

6 – Kwa ajili ya uponyaji wa nchi yetu

Uliwafanya watu, mwanamume na mwanamke, ili kuwa wawakilishi wako juu ya nchi, kuijaza na kutawala samaki wa baharini, ndege wa angani na juu ya kila kilicho hai kitambaacho juu ya nchi (Mwa 1: 26). Uliwapa pumzi watu walio juu ya nchi na roho wale waishio ndaji yake (Isa 42: 5; Mwa 2: 7). Uliwapa wanadamu chakula – kila

mche utoao mbegu na kila mti ambao matunda yake yana mbegu, na kila kilicho hai kitambaacho juu ya nchi, ulitupa kama chakula (Mwa 1: 29; 9: 3; Kum 12: 5). Ni wewe Bwana Mungu uifanyaye nchi kuzaa matunda, utoaye wingi wa nafaka na mvinyo. Unafurahisha mioyo yetu na divai, unatupa mafuta yang'aze nyuso zetu, na mkate unaoitia nguvu mioyo yetu (Mwa 1: 11; 27: 28, Zab 10: 14, 15). Wewe Bwana Mungu huinyeshea nchi na kuitengenezea mvua. Unatoa mvua kwa majira yake, mvua ya masika na mvua ya vuli (Zab 65: 9; 147: 8; Kumb 11: 14).

Unatamalaki juu ya nchi yote (Zab 97: 1), lakini umewapa wanadamu nchi kama mahali pa kukaa na kutawala (Zab 115: 6; Mwa 1: 26). Lakini unajua kila kitu kitokeacho duniani humu (Zek 4: 10; Zab 33: 13), ukichunguza baya na jema (Mit 15: 3). Wala hakuna kiumbe kisichokuwa wazi mbele zako lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pako, na ni kwako ndiko tunapasw kutoa hesabu (Ebr 4: 13). Tunaposimama mbele zako sasa, tunaungama kwamba sisi, watu katika jumuiya hii, tumeshindwa katika jukumu letu tulilopewa na Mungu. Nchi yetu imeharibiwa na kunajisiwa kwa sababu ya dhambi na uasi wetu dhidi yako (Mwa 6: 11 – 12; Isa 24: 4 – 6). Tafadhali uwe mwenye neema kwetu kama vile sisi, watoto wa Mungu, tunavyokugeukia wewe ili kuomba kwa ajili ya ukombozi wako mkamilifu (Rum 8: 19 – 23) na kwa ajili ya uponyaji wa jumuiya yetu na nchi yetu (2Nya 7: 13 – 15).

7 – Toba na hatia ya Damu

Bwana Mungu, Wewe ni mwenye rehema na mwenye neema, si mwepesi wa hasir ana mwingi wa upendo na uaminifu. Unasamehe uovu, makosa na dhambi (Kut 34: 6 – 7(. Uwe mwenye rehema kwetu kwa maana kuna mahali penye giza katika nchi, ikikaliwa na uovu na nchi yote imeharibika na kunajisiwa na dhambi (Zab 74: 20; Mwa 6: 11 – 12; Isa 24: 12). Nchi inazaa michongoma na miiba, na hata inawatapika watu (Mwa 3: 17, 18; Law 18: 25 – 28). Nchi zetu zimejazwa hukumu za damu, miji na majiji yetu yamejaa vurugu na uovu na sisi na vizazi vilivyopita tumechukulia maisha kwa heshima ndogo (Eze 7: 23; Hab 2: 12). Kwa sababu ya hatia ya damu iliyosababishwa na mauaji, vita na utoaji mimba, watu wengi wamekuwa wazururaji na wakimbizi (Mwa 4: 11, 12). Ardhi imelaaniwa na haitoi nguvu yake tunapoilima, mbingu zimekuwa kama shaba na nchi kama chuma (Mwa 4: 12; Kum 28: 23; Zab 107: 34). Unachukia mikono imwagayo damu na hujibu maombi ya wale wenye hatia ya damu mikononi mwao (Mit 6: 17; Isa 1: 15; 59:2). Ulisema kwamba uhai wa mtu uko katika damu na kwamba

damu yao inakulilia kwa ajili ya kulpiza kisasi (Mwa 4: 10; Law 17: 11).

Bwana, Mkombozi wetu, tafadhali utusamehe kwa ajili ya umwagaji damu wote katika taifa letu a katika jumuiya hii, ondoa laana ya umwagaji damu kutoka katika nchi yetu, utusafishe kabisa uovu wetu, na utuoshe na dhambi yetu (Yoe 3: 21; Zab 51: 2, 14). Unafanya vita vikome unapohukumu na kukemea mataifa (Zab 46: 9; Mik 4: 3). Uwe mwenye rehema na kuanzisha ufalme wako katika jumuiya yetu na nchi yetu ili kwamba Mfalme wa Amani atawale na kumiliki katikati yetu (Isa 9: 6, 7; Zek 9: 10; Rum 14: 17).

8 – Toba kwa ajili ya ibada ya sanamu.

Bwana wa majeshi. Wewe peke yako ndiwe Mungu. Wewe, ndiwe uliyeziumba mbingu na nchi (Isa 37: 16). Hapana Mungu mwingine zaidi yako, Mungu mwenye haki na Mwokozi (Isa 45: 21). Lakini wanadamu ingawa walikujua Wewe, hawakukuheshimu wala kukushukuru bali tulikuwa bure katika fikra zetu na mioyo yetu yenye ujinga ilitiwa giza. Sisi na vizazi vilivyopita tuliibadili kweli ya Mungu kuwa uongo na kuvisujudia vitu vilivyoumbwa badala ya Muumba (Rum 1: 21, 25). Watu wote walinyooshea miungu migeni mikono yao (Zab 44: 20). Kupitia ibada yetu ya sanamu, tamaa na kujiabudu, tumeinajisi nchi (Kol 3: 5; Zab 106: 38; Eze 22: 4; 36: 18). Ulisema ya kwamba tusijifanyie sanamu wala sanamu ya kuchonga, wala mnara au kujiwekea jiwe lililochorwa ili kulisujudia, kwa kuwa wewe ndiwe Mungu (Law 26:1).

Sasa ee Bwana, tunavuna matunda ya dhambi zetu. Ukame unatupiga, njaa inaangamiza watul vita vinasukasuka kati ya mataifa na majanga ya ikolojia yanaiteketeza nchi yetu kwa sababu tumetenda pasipo imani dhidi yako na kwenda mbali nawe (Eze 14: 12 – 21, Yer 2: 5). Bwana, tunatahayari juu ya njia zetu, maovu yetu yamefika juu ya vichwa vyetu na hatia yetu imeongezeka na kufika mbinguni (Eze 9: 6, 7). Tumetenda dhambi pamoja na baba zetu, tumetenda maovu na tumefanya ubaya, uturehemu na kutusamehe dhambi yetu (Zab 106: 6). Ututakase na uchafu wetu wote na vinyago vyetu vyote (Eze 36: 25, 26). Ondoa majina ya miungu mingine vinywani mwetu, inua kanisa safi na lisilo na waa ambalo litaonyesha hekima yako iliyodhihirishwa kwa falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho (Hos 2: 17; Efe 3: 10).

9 – Toba kwa ajili ya udhalimu na maagano yaliyovunjwa.

Mungu Mwenyezi na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, tunakupa ukuu. Wewe ni Mwamba, kazi yako ni kamilifu; njia zako zote ni haki. Wewe ni Mungu wa kweli na usiye na udhalimu (Kum 32: 3, 4). Haki na hukumu ni msingi wa kiti chako cha enzi; fadhili na kweli zahudhuria mbele za uso wako (Zab 89: 14, 15). Unamfanyia yatima na mjane hukumu ya haki; unampenda mgeni na unampa chakula na mavazi (Kum 10: 18). Umetuonyesha yaliyo mema, na unatutaka kutenda haki, kupenda rehema na kwenda kwa unyenyekevu kwa Mungu wetu (Mik 6: 8).

Mwamuzi wa dunia yote, twaja kuomba rehema na neema kwa ajili ya jumuiya yetu na nchi yetu. Haki i mbali nasi. Twajikwaa na kuanguka kwa sababu ya makosa yetu tuliyo nayo pamoja nasi, na tunayajua maovu yetu. Tumekukosea na kukudanganya, na kumwacha Mungu wetu. Tunanena Jeuri na uasi, tukikusujudia na kuyatoa moyoni maneno ya uongo. Mara nyingi hukumu hugeuzwa ikaenda katika mataifa yetu na haki husimama mbali sana. Kweli imeanguka katika njia kuu (Isa 59: 9 – 15). Nchi inaomboleza na imenajisiwa kwa watu wanaoikaa, kwa maana wameziasi sheria na wamelivunja agano na Wewe. Kwa hiyo laana imeila nchi yetu (Isa 24: 3 – 6). Tunajenga nyumba zetu wenyewe kwa uovu, tukitumia utumishi bila ujira (Yer 22: 13). Tuna sheria zisizo za haki na amri zenye kukandamiza, kuwafanya wajane kuwa mateka na kuwaibia yatima (Isa 10: 2). Tunatubu, tunaomba msamaha, tunakugeukia Wewe. Jaza mioyo yetu na kweli na haki na uiponye nchi yetu. Tunaomba hili katika Jina la Yesu.

10 – Toba kwa ajili ya ufisadi.
Bwana Mungu, tumeinajisi nchi kwa kuachana, kwa vitendo vya ngono vyenye kuchukiza kama vile ushoga, kujamiiana kwa maharimu, uasherati na ukahaba (Yer 3: 1 – 3; Rum 1: 25, 27, Law 18: 23). Tunaungama kwamba kizazi chetu kimejazwa na uovu, ufisadi, ubaya, tamaa, nia mbaya, husuda tele, mauaji, ugomvi, udanganyifu na hadaa. Kuna wasengenyaji, wenye kumchukia Mungu, wenye jeuri na watu wenye kiburi, wasioaminika, wasiopenda, wasiosamehe na watu wasio na rehema (Rum 1: 29 – 30). Hata katika Kanisa tunaungama kwamba tumeinajisi miili yetu kwa zinaa na kwa hivyo tumelinajisi hekalu la Roho Mtakatifu (1Kor 6: 18 – 20). Kama Wewe, Bwana ungehesabu maovu yetu, nani angesimama? Lakini kwako kuna msamaha, ili kwamba wewe uogopwe (Zab 130: 3 – 4). Ndiyo, rehema na msamaha ni kwa Bwana Mungu wetu, ingawa tumemwasi (Dan 9: 9).

Tunajinyenyekesha mbele zako na kuomba kwamba utatuongoza katika haki na kutufundisha nji azako (Zab 25: 9).

Utusaidie ili tusiishi kulingana na shauku zetu za mwili bali tuyafishe matendo ya mwili kwa Roho wako (Rum 8: 13). Tunataka kuenenda kwa Roho ili kwamba tusitimize tamaa za mwili (Gal 5: 16 – 26). Utusaidie ili tuutunze mwenendo wetu katik aheshima kati ya wasioamini ili kwamba wauone mwenendo wetu mwema na wakutukuze wewe (1Pet 2; 11 – 12). Utusamehe kwa kuwa na nia ya mwili na utusaidie tuweke nia zetu kwenye mambo ya Roho ili kwamba tukupendeze wewe (Rum 8: 5 – 6). Tunakuomba utugeuze kwa kufanya upya nia zetu kwa Neno lako, ili kwamba tusiifuatishe namna ya dunia hii, bali tupate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kupendeza na ukamilifu (Rum 12: 2).

11 – Tumwagie Roho Wako.

Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, asante kwamba ulitupa Roho Mtakatifu ili atufundishe, atuongoze na kutufariji (Yn 14:26). Asante kwamba kupitia Roho wako Mtakatifu, Roho wa kufanywa wana, (Rum 8: 15; Gal 4: 16), tunaweza kukujua wewe na kukuita "Aba Baba" na kwamba haujatuacha peke yetu bali umetupa Msaidizi (Yn 14: 16, 18; Yn 15: 26).

Tafadhali utusamehe kwa mara nyingi ambazo tumemhuzunisha na kumzimisha Roho Mtakatifu, au kukataa kutii njia zako na kumpinga (Efe 4: 30; 1The 5: 19; Mdo 5: 9). Utulinde kutoka kwenye kunena dhidi ya, kuasi au kumdanganya Roho Mtakatifu ili kwamba usitugeukie na kuwa adui yetu (Mt 12: 32; Mdo 5: 3; Isa 63: 10, 11). Utupe Roho wako wa hekima, ufahamu, uweza, ushauri na maarifa (Isa 11: 2) ili kwamba tuweze kulishirikisha Neno lako kwa ujasiri kwa watu wengine, hata kwa wale walio katika mamlaka (Dan 4: 9. 5: 11; Mdo 4: 8). Utujaze na Roho yako ili kwamba hata tunapoteswa, bado tuseme kweli na tusiwe kimya juu ya upendo wako na tumaini tulilo nalo katika mioyo yetu (Mdo 4: 31). Mimina upendo wako ndani ya mioyo yetu kupitia Roho Mtakatifu ili kwamba tuweze kupenda bila masharti (Rum 5: 5). Hukutupa roho ya woga bali ya upendo, nguvu na moyo wa kiasi (2Tim 1: 7). Acha tunda la Roho lionekane katika na kupitia maisha yetu (Gal 5: 22 – 23).

Roho wako Mtakatifu na auhakikishe ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki na hukumu (Yn 16: 7 – 8). Acha Kanisa liongezeke na kuenenda katika kicho cha Bwana na katika faraja ya Roho

Mtakatifu (Mdo (9: 31). Tutie nguvu na Roho wako Mtakatifu ili kwamba tuwe mashahidi wako hata miisho ya nchi (Mdo 1: 8).

12 – Watu wote na waisikie sauti Yako.

Baba yetu wa mbinguni, sauti yako I juu ya mataifa, sauti yako ina nguvu; sauti yako imejaa adhama, sauti yako inavunja mierezi, inavunjavunja mierezi ya Lebanoni. Sauti yako yaipasua miali ya moto! Sauti yako yalitetemesha jangwa. Sauti yako yawazalisha ayala na kuifichua misitu; na ndani ya hekalu lako (na mioyo ya watoto wako) kila mmoja husema "UTUKUFU!" (Zab 29: 1 – 9). Baba, ulisema: "Iwe Nuru!" na ikawa nuru (Mwa 1: 3). Kwenye giza la ulimwengu wetu, ulimtuma Mwanao, Neno lillofanyika mwili (Yn 1: 1 – 14). Yeye ni Nuru ya Ulimwengu ili kwamba tuweze kuona nuru, na kuwa na tumaini mioyoni mwetu (Efe 1: 18). Sauti yako toka mbinguni imetuamuru tumsikie Mwanao (Mk 9: 7). Yesu alisema kwamba Yeye ni Mchungaji Mwema, na kwamba kondoo wake wote wataijua sauti yake (Yn 10: 3 – 5; 14 – 16). Utusaidie kuipambanua kweli kutoka uongo na kuijua sauti yako kwa hakika (Yn 18: 13) na tunapoisikia sauti yako, utusaidie tusifanye migumu mioyo yetu na kukuasi. Tunaomba kwamba jumuiya na nchi yetu iisikie sauti yako, hata ingaw abaadhi ya watu wanakughadhibikia (Zab 46: 6). Acha wale wasiokujua wala kujali kukutii waone uweza wako na wainame mbele zako (Kut 5: 2). Tupe maneno yako ili kwamba tuwe sauti yako ili kusema kwa serikali na viongozi ili kuwasaidia kuenenda katika njia zako (Mk 3: 11). Utusaidie kuja karibu nawe ili kupokea jumbe unazotaka kutoa kupitia Kanisa lako kwenda kwa ulimwengu (Kum 5: 25 – 27). Tupe pia uwezo wa kuinena na kuitafsiri Injili kwenye lugha za mioyo ya watu wote (Mdo 2: 11). Utusaidie kuja karibu sana nawe kwamba tuzisikie shauku za moyo wako na kujitoa wenyewe kwa utumishi wako (Isa 6: 8)

13 – Kwa ajili ya mahusiano katika kanisa.

Bwana Yesu Kristo, Wewe ni kichwa cha Mwili, Kanisa. Tunaungama kama Kanisa kwamba hatujaupambanua Mwili wkao kwa usahihi bali tumejifikiria wenyewe zaidi sana kuliko tunavyopaswa, tukisahau kwamba ni Mwili mmoja wenye viungo vingi na kwamba viungo vyote havina kazi moja, lakini bado kila kiungo kinahusika kwa vingine vyote (Rum 12: 3 – 5). Tunaungama kwamba tumejivunia mawazo yetu wenyewe na hivyo kama Mwili tumeteseka na kutenganishwa na hatukuweza kukua kifikia

kupevuka (Kol 2: 18 – 19). Tumeendelea kuumana na kulana na baadhi ya viungo viliharibiwa kwa ukosefu wa upendo (Gal 5: 14 – 15).

Tafadhali utusamehe na kurejeza mahusiano yetu. Uliviungamanisha viungo vya Mwili wkao ili kwamba kusiwepo na faraka, bali kwamba tutunzane kila kiungo na mwenziwe, na kuteseka pamoja na pia kufurahi wakati viungo vingine vinapotukuzwa (1Kor 12: 24 – 27). Tuwe na umoja kama Wewe na Baba mlivyo umoja. Maombi Yako na yajibiwe kwamba Baba atulinde kwa uweza wa Jina lake, Jina ulilopewa, ili kwamba umoja wetuudhihirike katika upendo ambao tunao kila mmoja kwa mwenzake (Yn 17:11), kwa vile ni kupitia upendo huu ndipo ulimwengu utajua kwamba sisi ni wako (Yn 13: 35).

Tunaomba kwamba uturejeze sisi, Kanisa, kwenye kusudi ulilokuwa nalo kwa ajili yetu kabla hujatuumba (Efe 2: 15; 3: 10, 11). Tunapokubaliana sisi kwa sisi, Jina lako na Litukuzwe (Rum 15: 7).

14 – Damu ya Yesu Kristo

Kulingana na Maandiko vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo la dhambi (Ebr 9: 22). Tunakuja kwako Bwana Yesu kama Mpatanishi wa agano jipya (Ebr 12: 24). Asante kwa kuonyesha upendo wako kwetu, kwamba tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu (Rum 5: 8). Ndiyo, ulikwisha kumweka kama dhabihu ya upatanisho na kwa damu yake ulionyesha haki yako kwa maana Kristo alikuja kama Kuhani Mkuu na kwa damu yake mwenyewe aliingia Patakatifu sana mara moja tu na kupata ukombozi wa milele (Rum 3: 25), Ebr 9: 11 – 12). Kwa damu ya thamani ya Kristo, kama ya mwana-kondoo asiye na hila na asiye na waa. Ulitukomboa na kusamehe dhambi zetu sawasawa na wingi wa neema yako (1Pet 1: 18 – 19; Efe 1: 7; Kol 1: 14). Sasa sisi, ambao hapo kwanza tulikuwa mbali na wafu katika makosa na dhambi zetu, tumeletwa karibu na kiti chako cha enzi kwa damu ya Kristo (Efe 2: 5, 13). Ni kupitia damu ya Kristo ambapo tunahesabiwa haki na kupatanishwa nawe, Baba yetu wa mbinguni (Rum 5: 9; Kol 1: 20.

Ni damu yako ndiyo isafishayo dhamiri zetu kutokana na matendo mafu ili tumtumikie Mungu aliye hai (Ebr 9: 14). Ulitupenda na ukatusafisha dhambi zetu katika damu yako ili kwamba tusafishwe dhambi yote (Ufu 1: 5; 1Yoh 1: 7) na ulitutakasa katika Roho kwa

damu yako (Ebr 13: 12; 1Pet 1: 2). Ni kupitia damu yako ambapo tunamshinda shetani (Ufu 12: 11).

Utufanye wakamilifu katika kila tendo jema kwa damu ya agano la milele, ili tuyafanya mapenzi yako. Fanya ndani yetu lipendezalo mbele zako, kwa Yesu Kristo, utukufu una yeye milele na milele. Amen (Ebr 13: 20 – 21).

15 – Kwa ajili ya kanisa ili kutimiza kusudi lake.

Baba, Kristo na afunuliwe na kujulikana kupitia Kanisa ili kwamba mataifa yote yaweze kumwamini na kumtii Mwanao (Rum 16: 25 – 27). Acha ushuhuda wa Yesu Kristo uthibitishwe katika na kupitia kanisa. Tunapomngojea Bwana wetu Yesu Kristo kufunuliwa, tusipungukiwe na karama yo yote ya roho ili kufanya kazi yako. Tuthibitishe hata mwisho ii kwamba tusilaumiwe siku ile ya Bwana wetu Yesu Kristo (1Kor 4 – 8).

Baba, kwa shukrani na sana ninaomba kwa ajili ya kuongezeka upendo na amani katika kanisa. Tafadhali Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, tupe Roho wako wa hekima na ufunuo, ili kwamba tuweze kukujua na kukufanya ujulikane na watu katika jumuiya yetu. Tunaomba pia kwamba macho ya mioyo yetu yatiwe nuru ili kwamba tuweze kujua tumaini la mwito wako jinsi lilivyo, na utajiri wa utukufu wa urithi katika watakatifu jinsi ulivyo, na ubora wa ukuu wa uweza wako jinsi ulivyo kwetu sisi tuaminio (Efe 1: 15 – 23).

Tafadhali, ulirejeze kanisa kama nyumba ya maombi ili kwamba kanisa lijitoe tena kwa maombi, likeshe na kuwa na shukrani (Kol 4: 2). Tunaomba kwa juhudi kwamba utaturuzuku kile kinachokosekana katika imani yetu. Bwana na uufanye upendo wetu uongezeke na kufurika kwa ajili ya sisi kwa sisi na mwingine ye yote. Na uifanye imara mioyo yetu ili kwamba tusiwe na lawama na tuwe watakatifu katika uwepo wako (1The 3: 9 – 13). Baba tunaomba kwa kujiamini kwamba Wewe uliyeanza kazi njema ndani yetu sote, utaiendeleza hata siku ya Kristo Yesu (Flp 1: 6 – 11).

16 – Kwa ajili ya kicho cha Bwana.

Bwana Mungu Mwenyezi, unapaswa kuhofiwa kuliko miungu ote (1Nya 16: 25 – 26). Bwana, unataka utii na mioyo ambayo imejitoa kabisa kwako peke yako. Tunataka kukucha Wewe pekee, na

kukutumikia katika kweli kwa mioyo yetu yote, kwa maana umefanya mambo makuu kwa ajili yetu (1Sam 12: 20 – 24).

Bwana Mungu, kukucha wewe ndio mwanzo wa hekima (Zab 111: 10). Tunaomba utupe hekima (Yak 1: 5) na utukumbushe kukucha wewe. Macho yako, Bwana, ya juu ya hao wakuchao, na juu ya wale wanaotumainia rehema zako, ili kuwaokoa nafsi zao na mauti, na kuwahuisha wakati wa njaa. Nafsi zetu zinakungoja Wewe, kwa maana wewe ndiwe msaada wetu na ngao yetu (Zab 33: 18 – 22). Bwana wafana kituo kuwazunguka wale wakuchao na kuwaokoa. Na tuuonje wema wako, kwa maana unawaita heri wale wakutumaino! (Zab 34: 7 – 10).

Watu wote katika jumuiya yetu na katika nchi yetu na wamche Bwana. Wote wakaao dunani wakuche wewe (Zab 33: 8). Roho wako wa Hekima na Roho wa kumcha Bwana na afanye kazi kwa nguvu ndani yetu (Isa 11: 2). Watu katika jumuiya na nchi yetu na wasiidharau hekima yako na wachague kukucha wewe.

Unaturuhusu kuwa na njaa kwa ajili Yako, ili tujue kwamba mtu hawezi kuishi kwa mkate tu, bali mtu huishi kwa kila Neno litokalo kinywani mwako. Umeturudi ili tuenende katika njia zako na kukucha wewe (Kum 8: 3 – 6). Utufundishe njia zako ili tuenende katika kweli yako. Tupe moyo usiogawanyika ili kulicha Jina lako (Zab 86: 11). Utusaidie kuondokana na uovu na kutenda mema, kutafuta amani na kuifuatia na kuzuia midomo yetu kusema hila (Zab 34: 13 – 14). Leo tunachagua wenyewe kwamba tutamcha Bwana na kukutumikia wewe pekee katika uaminifu na katika kweli (Yos 24: 14 – 15).

17 – Kwa ajili ya makusidi yako kwa familia na watoto.

Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, tunapiga magoti mbele zako, ambaye kila familia duniani inaitwa (Efe 3: 14, 15). Kwa vile familia zote zina mwanzo wao katika wewe, tunakuomba ulete uponyaji na urejezo kwa familia katika jumuiya yetu. Tunakiri na kuungama kwamba maumivu mengi ambayo familia zinapitia ni kwa sababu ya njia zetu za dhambi. Tunaungama kwamba hatujaishi kulingana na viwango vyako katika ndoa zetu na katika kuwalea watoto wetu (Isa 1: 23). Tumepuuzia amri yako kwamba waume wanapaswa kuwapenda wake zao kama Yesu anavyolijali Kanisa, na kwamba wake wanapaswa kuwatii na kuwastahi waume zao kama Kanisa linavyomtii Yesu (Efe 5: 22 – 33; 1Pet 3: 7).

Kupitia damu yako tunaweza kupatanishwa sisi kwa sisi (2Kor 5: 18). Uturehemu. Pia tunaungama kwamba kama watoto hatuna utii kwa wazazi wetu na hatuwaheshimu kama ulivyotuamuru kufanya (2Tim 3: 2; Kut 20: 12). Kama akina baba na akina mama hatujaweka vielelezo kwa ajili ya watoto wetu kama kwa mitindo ya maisha ya kumcha Mungu. Tuliwasababishia kujikwaa na tuliwachokoza, na hatukukupa utukufu kwa kuwaambia juu yako (Zab 78: 4 – 8). Tunahitaji utakaso na uponyaji wako, uje na usafishe familia zetu kwa Neno lako (Efe 5: 26). Tuokoe na uovu, ondoa mashina yote ya uchungu, chuki na kutokusamehe kati yetu. Uyafanye mahusiano yetu sisi kwa sisi kuwa mazuri tena.

18 – Kwa ajili ya uponyaji wa Kristo.

Tunakuhimidi Bwana, na kukumbuka yote uliyotutendea, ni wewe ndiwe unayesamehe dhambi zetu na kuponya magonjwa yetu yote (Zab 103: 2 – 3). Wewe ndiwe Mungu Mponya wetu (Kut 15: 26). Umetupa Mwanao, Yesu Kristo ili kuchukua masikitiko yetu na kujitwika huzuni zetu. Alijeruhiwa kwa makosa yetu, na alichubuliwa kwa maovu yetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Baba uliweka dhambi zetu zote juu yake. Yalikuwa ni mapenzi yako kwa Yesu kuteseka, na uliifanya nafsi yake sadaka kwa ajili ya dhambi. Kwa kuwa alichukua dhambi ya ulimwengu, aweza sasa kuwaombea wenye dhambi (Isa 53: 1 – 12).

Ulimtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na kwa nguvu ili kuihubiri Injili ya ufalme, na kuponya wagonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu, hata kuponya kutoka kwenye uonevu wa kipepo (Mt 4: 23 – 24; Mdo 10: 38). Jua la Haki kwa hakika limezuka lenye kuponya katika mbawa zake (Mal 4: 2). Bwana Yesu Kristo, jumuiya yetu inahitaji uponyaji wako. Uje uponye nafsi na miili yetu maana tumekutenda dhambi (Zab 41: 4). Ponya mioyo iliyovunjika, tangaza uhuru kwa wale waliotiwa utumwani na dhambi, na kufungwa magereza ya wale waliofungwa na desturi mbaya, utumwa wa kujitaabisha mioyo iliyoharibiwa na ngome za kiroho (Isa 6: 1). Umeahidi kwamba kama sisi tulioitwa kwa Jina lako tutajinyenyekesha, na kuomba na kuutafuta uso wako, na kuziacha njia zetu mbaya, basi utasikia kutoka mbinguni, utasamehe dhambi yetu na kuiponya nchi yetu (2Nya 7: 14). Taifa letu linahitaji uponyaji. Timiza ahadi zako ili kuleta uponyaji, vile tunavyojinyenyekesha mbele zako.

19 – Kwa ajili ya wanaotaabika na kuteseka.

Bwana Yesu Kristo, umetuita ili kufuata nyayo zako, hata katika mateso. Ulitukanwa na kuteswa kidhalimu lakini kamwe hukulipiza kisasi, ulichagua badala yake kujikabidhi kwake yeye ahukumuye kwa haki (1Pet 2: 21 – 24). Mateso yako yalilazimu ili tuweze kupokea msamaha wa dhambi (Lk 24: 46 – 47) na kwa sababu ya utii na utayari wako wa kuteseka, tumetangazwa wenye haki. Uliwaita heri wale wanaoteswa kwa ajili ya haki, na ukatuahidi thawabu kuu mbinguni tunapowabariki wale wanaotutesa na kutuudhi, kwa sababu ya Jina lako (Mt 5: 10 – 12). Utusaidie tuwe na nia kama yako, ili tuishi kwa mapenzi ya Mungu (1Pet 4: 1, 19) na kama hiyo inajumuisha kuteseka, kwamba kama Kanisa la kwanza, tutafurahi kwa sababu tunahesabiwa kustahil ikuteseka kwa ajili ya Jina lako (Mdo 5: 41; Flp 1: 29; 2The 1: 5 – 6). Utusaidie kuelewa kusudi la kuteseka, kwa vile Paulo alitangaza kwamba wote wanaopenda kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu watateseka (Rum 8: 17; 2Tim 3: 12). Utusaidie kusema kama Paulo: "Yote tunayotaka ni kukujua wewe, na uweza wa kufufuka kwako, na ushirika wa mateso yako, ili kuifikia kiyama ya wafu (Flp 3: 10 – 11).

Tunawaombea wale wanaotaabika na kuteswa kwa ajili ya Jina lako, kwamba utaukamilisha, kuwathibitisha na kuwatia nguvu (1Pet 5: 10). Tupe ujasiri kunena Neno lako hata wakati tunapotishwa na kuteswa (Mdo 4: 29). Utusaidie kujifunza utii kutokana na mambo tunayoteseka kwayo (Ebr 5: 8). Tunawaombea wale wanaolitesa Kanisa lako.

20 – Kwa ajili ya serikali yetu.

Bwana, unabadili nyakati na majira; unawaweka wafalme na kuwaondosha madarakani (Dan 2: 20 – 22). Kwa maombi, maombezi na kutoa shukrani tunakuja mbele ya kiti chako cha enzi kwa ajili ya wafalme, serikali yetu, na wote wale walio katika mamlaka, kwamba tuishi kwa amani na maisha ya utulivu katika utauwa wote na utakatifu – maana hili ni zuri, na tena linakupendeza Mungu Mwokozi wetu, unayetaka watu wote waokolewe na kupata kujua yaliyo kweli (1Tim 2: 1 – 4). Mioyo ya watawala wetu ipo mikononi mwako, iongoze kama mfereji wa maji popote upendapo (Mit 21: 1). Uwaondoe washauri wabaya katika uwepo wa viongozi wa serikali, rais, mawaziri na wakuu wengine, na uithibitishe serikali yetu katika haki na kweli (mit 25:5). Ondoa ulafi kutoka katika mioyo yeo na uwalinde na kuchukua rushwa (Mit

29: 4). Serikali yetu na ishughulikie maskini kwa uaminifu na haki (Mit 29: 14).

Mwonyeshe rais na wakuu wote wa serikali yaliyo mema na yale unayotaka kwao. Fanya mioyo yao kutenda haki na kupenda rehema na kwenda kwa unyenyekevu katika uwepo wako (Mik 6: 8). Bwana Mungu, jaza mioyo ya watawala wetu na upendo na uaminifu ambao utawahifadhi salama na kwa njia hii tutakuwa na usalama na amani (Mit 20: 28). Na umtume Roho wako Mtakatifu kwenye majengo ya serikali na mahali ambapo watawala wetu wanakusanyika, kupitisha sheria na kufanya maamuzi, ili kuhakikisha kwa habari ya dhambi palipo ulazima na kuwathibitisha katika kweli na haki (Yn 16: 8 – 11). Tunaiombea serikali yetu kwa ajili ya ulinzi dhidi ya nguvu za giza na kwamba hawatahusika na uchawi , ibada ya sanamu au namna yoyote ya mizungu. Kama kanisa, tunampinga ibilisi mahali ambapo hujaribu kushambulia, kutega na kuidanganya serikali (Yak 4: 7)

21 – Ili kujazwa na Neno lako.

Kwa Neno lako mbingu zilifanyika (Zab 33: 6) na unavishikilia vitu vyote kwa uweza wa Neno lako (Ebr 1:3) Neno lako li hai tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao ukatao kuwili, likichoma hata kugawana nafsi na roho, tena linatambua mawazo na makusudi ya moyo (Ebr 4: 12). Neno lako pia ni kama moto na nyundo ivunjayo jiwe vipande vipande (Yer 23: 29). Neno lako ni upanga wa Roho (Efe 6: 17) na kila Neno litokalo kinywani mwako halitakurudia bure, bali litatimiza mapenzi yako nalo litafanikiwa katika mambo yale uliyotuma (Isa 55: 11).

Wewe, unayejifunua kwa Neno lako (1Sam 3: 21), fungua akili zetu tupate kuelewa Maandiko (Lk 24: 45) na utupe Roho wako wa hekima na ufunuo ili kukujua Wewe (Efe 1: 17). Neno lako na liwe taa ya miguu yetu na mwanga wa njia yetu (Zab 119: 105). Uzielekeza hatua zetu kwa Neno lako (Zab 119: 133). Na tuishi kwa kila Neno litokalo kinywani mwako (Kum 8: 3; Mt 4: 4). Neno lako na litusafishe (Yn 15: 3; Efe 5: 26). Neno lako na lituponye na kutuokoa kutoka katika maangamizo (Zab 107: 20).

Neno lako na likae kwa wingi ndani yangu ili niweze kuwafundisha na kuwatia moyo wengine (Kol 3: 16) na kumshinda yule mwovu (1Yon 2: 14). Kusikia Neno lako na kulete imani kwenye moyo wangu (Rum 10: 17).

Ulithibitishe Neno lako katika miji na mataifa yetu, na likue kwa nguvu na kushinda (Mdo 19: 20). Mwili wote ni kama majani, na fahari yake yote ni kama ua la majani. Majani hukauka na ua lake huanguka, bali Neno la Bwana ladumu hata milele (1Pet 1: 24 – 25).

22 – Ili kumshinda yule mwovu.

Lilikuwa ni kusudi lako la milele, ambalo ulilifanikisha katika Yesu Kristo Bwana wetu, ili hekima yako iliyo ya namna nyingi ijulikane na kanisa kwa falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho (Efe 3: 10). Tunaomba kwamba utaponya waliovunjika moyo katika jumuiya yetu, kwamba utawaweka huru mateka, kuwapa vipofu kuona na kwamba utawaacha huru wote wale wanaosetwa (Lk 4: 18). Ulimpa Mwanao mamlaka yote mbinguni na duniani, kwamba kwa Jina la Yesu Kristo, kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri kwamba Yeye ni Bwana (Mt 28: 18 – 20, Flp 2: 10, 11) Hili na litokee katika jumuiya yetu.

Kazi za Ibilisi na ziharibiwe katika jumuiya yetu, kwa sababu kwa kusudi hili Mwanao alikufa (1Yoh 3: 8). Iokoe jumuiya yetu kutoka katika nguvu za giza (Kol 1: 13 – 14). Kulingana na Neno lako, macho ya wasioamini katika jumuiya yetu na yafunguliwe ili wageuke kutoka gizani hadi nuruni, na kutoka kwenye nguvu ya shetani hadi kwa Mungu ili wao pia waweze kupokea msamaha wa dhambi na uridhi miongoni mwa wale wanaotakaswa kwa imani katika Wewe (Lk 9: 1 – 2), Mt 28: 18 – 19; Mdo 26: 17 – 18). Mungu wa amani, tunaomba kwamba utamseta shetani chini ya miguu yetu upesi (Rum 16: 20). Asante kwa kutupa silaha za Mungu, ili tuweze kuzipinga hila za Ibiisi tunaposhindana na falme na mamlaka juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Tunatangaza kwamba aliye ndani yetu ni mkuu kuliko yeye aliye katika ulimwengu (1Yoh 4: 4).

23 – Kwa ajili ya Ubaba wa Mungu kufunuliwa.

Baba wa milele, Wewe ni Muumba wetu uliyetufanya na kutuumba (Kum 32: 6). Sisi tu udongo, wewe ni mfinyanzi, sisi tukazi ya mkono wako (Isa 64: 8) Kwa hiyo pamoja na wingi wa mamilioni ulimwenguni tunakiri: Tunamwamini Mungu Baba, Mwenyezi, Muumba mbingu na nchi. Asante kwa ahadi yako ya agano kwamba utakuwa Baba kwetu na kwamba tunaweza kuwa wanao

wa kiume na wa kike (2Kor 6: 18). Jifunue kwa jumuiya yetu kama Baba, Yeye ambaye kutoka kwake hushuka kila kutoa kuliko kwema na kila kitolewacho kilicho kamili, na ambaye kwake hakuna badiliko wala kivuli cha kugeukageuka (Yak 1: 17). Na tukujue Wewe kama ulivyo kiuhalisi (1Yoh 2: 13 – 14). Kama Ibrahimu na Musa uliosema nao uso kw auso, tunataka kuishi nawe katika uhusiano wa uso kw auso.

Kama mwana anavyomheshimu baba yake na mtumishi bwana wake, tunataka kukuheshimu na kukustahi wewe (Mal 1: 6). Na kama Mwanao Yesu alivyokutukuza mbele ya ulimwengu (Yn 17:4).

Jifunue kama Baba wa yatima, Mtetezi wa wajane (Zab 68: 5). Hatukupokea kutoka kwako roho ya utumwa iletayo hofu bali tulipokea kutoka kwako Roho ya wana – Roho ya kufanywa wana. Na kwa Roho huyu pia twalia "Aba, Baba!" (Gal 4: 5 –7; Rum 8: 15, 17).Tunataka kuwa waabuduo halisi, kw ahiyo utufundishe, Baba, kukuabudu katika Roho na kweli (Yn 4: 23)./

24 – Kwa ajili ya wokovu wa wale wasiookoka.

Baba, ufalme wako na uje, mapenzi yako na yatimizwe duniani kama huko mbinguni (Mt 6: 10). Tunaomba kwa ajili ya wokovu wa watu kutoka kila taifa, kabila, jamaa na lugha – pia kwa ajili ya watu katika jumuiya yetu – kwamba wingi wa watu usiohesabika siku moja utasimama mbele ya kiti cha enzi mbele za Mwana-Kondoo (Ufu 7: 9).

Tunaombea mataifa ya ulimwengu na marafiki na majirani zetu wasiookoka ili wapatanishwe na wewe. Tunaomba hili kwa sababu hufurahii kufa kwake mtu mwovu, bali unafurahi wanapoghairi na kuziacha njia zao (Eze 18: 23).

Bwana Yesu, Wewe ni Mwana-Kondoo wa Mungu uichukuaye dhambi ya ulimwengu! (Yn 1: 29). Geuza mioyo ya wale wasiookoka kwako ili waweze kukugeukia Wewe (Omb 5: 2) kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu tunaomba kwamba utawahakikishia watu wa jumuiya yetu hatia kwa habari ya dhambi na haki na hukumu (Yn 16:8). Maelfu katika kanisa lako na waitikie utakapoita: "Nimtume nani? Na wawe tayari kwenda. Na waseme kama Isaya: "Mimi hapa. Nitume mimi!" (Isa 6: 8). Tunaona kwamba mavuno ni mengi na watenda kazi ni wachache. Basi tunakuomba, Bwana wa mavuno, peleka watenda kazi katika mashamba ya mavuno (Mt 9: 37 – 38). Wakristo ulimwenguni mwote na wainue macho yao ili

waone kwamba mashamba yako tayari kwa mavuno (Yoh 4: 35). Kanis ana lishike kwa njia mpya kwamba wito wetu ni kwenda ulimwenguni kote na kuhubiri habari njema kwa viumbe vyote (Mk 16: 15). Bwana Mungu, tunakuomba utende kwa ishara na ajabu na miujiza na karama mbalimbali za Roho Mtakatifu, zikigawanywa kulingana na mapenzi yake (Ebr 2: 1).

25 – Kwa ajili ya ufalme wako uje.

Baba, tunakuomba kwamba ufalme wkao uje na mapenzi yako yatimizwe duniani kama huko mbinguni (Mt 6: 9 – 10). Kutoka katika mataifa yote tutanena utukufu wa Ufalme wako na kuuhadithia uweza wako ili kuujulisha kwa wana wa watu matendo yako makuu, na utukufu wa fahari ya Ufalme wako. Ufalme wako ni Ufalme wa milele, na mamlaka yako yadumu kwa vizazi vyote (Zab 145: 11 – 13).

Utusamehe kwa kulenga zaidi kwenye mahitaji yetu wenyewe na kwenye kujenga falme zetu wenyewe. Tafadhali fungua macho ya mioyo yetu ili tuweze kujua tumaini ulilotuitia, na utajiri wa utukufu wa urithi wako ndani yetu, watakatifu, na ubora wa ukuu wa uweza wako kwa ajili yetu tuaminio (Efe 1: 18 – 19). Tunapiga magoti yetu na kukubal imamlaka ya Jina la Yesu na kukiri kwamba Yesu Kristo ni Bwana (Flp 2: 10 – 11).

Tunaomba kwamba wengi zaidi watasikia Neno la Injili ya Ufalme, na kwamba mbegu itadondoka katika mioyo iliyoandaliwa, ili kwamba kuwepo mavuno mengi ya roho katika kizazi chetu (Mt 13: 3 0 23). Sasa tunatangaza kwa mataifa yote: *"Inueni vichwa vyenu enyi malango, na inuliweni enyi malango ya milele, ili Mfalme wa Utukufu apate kuingia* (Zab 24: 7).

Tunakubariki Wewe, Mungu Uliye Juu sana, na kukusifu na kukuheshimu wewe uishiye milele (Dan 4: 34). Mamlaka yakoni mamlaka ya milele ambayo hayatapita kamwe na ufalme wkao ni ule usioweza kuangamizwa. Watakatifu wako ee Mungu Uliye Juu sana, wataupokea na kuumiliki huo Ufalme milele (Dan 7: 9, 10, 13, 14, 18). Kwako wewe uketiye juu ya kiti cha enzi na kwa Mwana-Kondoo, iwesifa, na heshima na utukufu na uweza, milele na milele (Ufu 5: 13).

26 – Utuokoe na yule mwovu.
Bwana Yesu, ulitufundisha kwamba: Usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu (Mt 6: 13). Kwa kifo cha ufufuo wako

ulishinda nguvu zote za uovu (Kol 2: 13 – 15). Ulitangaza kwamba milango ya kuzimu haitalishinda Kanisa lako (Mt 16: 19). Tunaomba kwa ajili ya kuokolewa kutoka kwenye uonevu wa kipepo. Tunaomba kwa ajili ya kuangusha ngome z auovu na itikadi zinazozuia kuenea kwa maarifa ya Mungu. Tunaupinga mpango wa shetani wa kuyaweka mataifa gizani (Yak 4: 7). Tunaomba kwamba utaondoa utaji unaowafunika watu na kuwaweka gizani (Mdo 26: 17 – 18(. Neno lako lilitangaza kwamba hakuna kitu, hata falme na mamlaka, kitakachoweza kututenga na upendo wako (Rum 8: 38 – 39). Tunaomba kwa ajili ya milango iliyofunguka ili Injili iweze kuingia katika kila taifa (Ufu 3: 8). Zuia uovu unaosaidia kuanzisha virugu na kifo. Vunja mshiko wa utumwa na udhalimu. Utujaze na Roho wako ili tulihubiri Neno lako pasipo hofu na kwa uaminifu (Mdo 1: 8). Tupe Roho yako ya maombi na kulalama ili kulia kwa niaba ya waliopotea (Zek 12: 10).

Kwa kuwa ufalme ni wkao na nguvu na utukufu hata milele na milele. Tunatangaza kwa mataifa yote: "Inueni vichwa vyenu, enyi malango ya mataifa, na inuliweni enyi malango ya milele, ili Mfalme wa Utukufu apate kuingia (Zab 24: 7).

27 – Kwa ajili ya Maskini na wahitaji.

Baba, tunaomba kwa ajili ya maskini wote katika jumuiya yetu na katika nchi. Neno lako linatufundisha kwamba siku zote kutakuwa na watu maskini katika nchi na unatuamuru tuwafumbulie mikono yetu maskini na wahitaji katika nchi yetu (Kum 15: 11).

Na uwainue maskini katika jumuiya yetu kutoka mavumbini na kuwapandisha wahitaji kutoka jaani (1Sam 2: 87). Bwana, uwe kimbilio la maskini wakati watenda maovu wanapojaribu kukatisha tamaa mipango yao (Zab 14: 6). Baba, na uwasikie maskini wanapokuita, uwaokoe na taabu zao zote (Zab 34: 6). Ni nani aliye kama Wewe, Ee Bwana Unawaokoa maskini na wale ambao wana nguvu kuliko wao, maskini na wahitaji na wale wanowaibia (Zab 35: 10). Watetee wanyonge na yatima; dumisha haki za maskini na wanaoonewa (Zab 82: 3). Faida ya watu maskini na isiondolewe kwa udhalimu (mt. 13: 23). Tunaliombea kanisa katika jumuiya na nchi yetu ili litoe kwa ukarimu kwa maskini. Wakristo na wasio wakristo na waelewe kwamba amhurumiaye maskini humkopesha Bwana, na kwamba Bwana atampa thawabu kwa lile alilotenda (Mit 19: 17). Tunaomba kwa ajili ya Wakristo zaidi kujali juu ya haki kwa maskini (Mit 29: 7), kuwanenea maskini, kuhukumu kwa haki na kutetea haki za maskini na wahitaji (Mit 31: 9). Utupe utayari na

shauku mpya kushiriki chakula chetu na wenye njaa na kuwapa hifadhi wale wasio na mahali pa kujisetiri na kuwavika walio uchi (Isa 58: 7). Habari njema na ihubiriwe kwa maskini (Mt 11: 5), maskini na wahitaji na walisifu jina lako (Zab 74: 21).

28 – Kwa ajili ya Kanisa.

Bwana Mungu, tunaomba kwamba Wewe, unayetoa sabur na kutia moyo, utupe roho ya umoja kati yetu wenyewe tunavyomfuata Kristo Yesu, ili kwamba kwa moyo mmoja na kinywa kimoja tupate kukutukuza Wewe, Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo. Utusaidie tukaribishane sisi kwa sisi kama naye Kristo alivyotukaribisha, ili kuleta sifa kwako (Rum 15: 5). Bwana wa tumaini na utujaze furaha na amani yote tunavyokuamini Wewe ili tupate kufurika katika tumaini na nguvu za Roho Mtakatifu (Rum 15: 13).

Baba wa huruma na Mungu wa faraja yote, utufariji katika dhiki zetu zote, ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki kwa faraja ambazo sisi wenyewe tumezipokea kutoka kwako (2Kor 1: 3 – 5). Nasi tunaomba kwamba Wakristo wasifanye lolote lililo baya (3Kor 13: 7). Maombi yetu ni kwa ajili ya kukamilika kwenu ili mfanywe kuonekana kwa waaminio (2Kor 13: 9). Tutaendelea kuomba mpaka Kristo aumbike ndani yao waaminio (Gal 4: 19).

Baba, tunaomba kwamba upate kutufanya imara kwa nguvu kupitia Roho wako katika utu wetu wa ndani, ili Kristo akae mioyoni mwetu kwa imani. Na kwamba tuwe na sheria na msingi katika upendo, na kwamba tuwe na nguvu, pamoja na watakatifu wote, tupate kufahamu jinsi ulivyo upana na urefu wa kimo na kina cha upendo Kristo, na kuujua upendo huu upitao ufahamu. Na kwamba tupate kujazwa kwa kipimo cha utimilifu wote wa Mungu. Sasa kwako Wewe uwezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo na tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu, utukuzwe katika Kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele (Efe 3: 14 – 21).

29 – Kwa ajili ya Kanisa.

Baba, tunawaombea waumini wote, kwamba wakati wowote tunapofumbua vinywa vyetu, maneno yapate kutolewa kwetu ili pasipo hofu tuijulishe ile siri ya Injili (Efe 6: 18 – 20). Na tunaomba pia, kwamba upate kufungua mlango kwa ajili ya ujumbe wetu, ili tuweze kutangaza siri ya Kristo. Tunaomba kwamba tupate

kuitangaza kwa dhahiri kama ipasavyo (Kol 4: 3 – 4). Baba, tunaomba pamoja na watakatifu wote kwamba sisi tunaotangaza hilo Neno tulindwe na wasioamini na kwamba maneno yetu yatakubalika kwa wote watakaolisikia (Rum 5: 30 – 32). Tunaomba kwamba sisi tunaoihubiri Injili tupate kuthibitika sana katika mapenzi ya Mungu (Kol 4: 12). Bwana, hukutupa roho ya uoga, bali ya nguvu, na ya upendo na ya moyo wa kiasi (2Tim 1: 7). Baba, tunaomba kwamba utamwaga Roho yako ya maombi na kulalama juu yetu ili tujitoe wenyewe kwa maombi, tukikesha katika kuomba huku na kushukuru (Kol 4: 2). Tunaomba kwa ajili ya Kanisa ambalo litamlilia Mungu usiku na mchana na kwamba mtatutendea haki, kwamba utayatengeneza yale yasiyo sahihi katika jumuiya yetu kama ulivyotuahidi (Lk 18: 7; 1The 3: 9 – 13).

Asante Baba kwamba tunaweza kuamini kwamba Wewe uliyeanza kazi njema ndani yetu utaiendeleza mpaka kuimaliza hata siku ya Kristo Yesu. Na haya ndiyo maombi yetu, kwamba pendo letu lizidi kuwa jingi sana katika maarifa na kina cha umaizi, ili tupate kuweza kupambanua yaliyo bora zaidi na tupate kuwa safi na bila lawama mpaka siku ya Kristo, hali tumejazwa matunda ya haki inayokuja kwa njia ya Yesu Kristo – kwa utukufu na sifa ya Mungu (Flp 1: 6 – 11).

30 – Kwa ajili ya Kanisa.

Bwana, kwa sababu uko karibu hatutajisumbua kwa jambo lolote, bali katika kila jambo kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, tuziwasilishe haja zetu kwako. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, ihifadhi mioyo yetu na nia zetu katika Kristo Yesu (Flp 4: 5 – 7). Bwana, kama kanisa tunaomba kwamba ukidhi mahitaji yetu yote kwa kadiri ya utajiri wako, katika utukufu ndani ya Kristo Yesu (Flp 4: 19 – 20). Bwana, Wewe umpaye mbegu mwenye kupanda na mkate kwa chakula, tunaomba kwamba utatupa pia na kuizidisha ghala yetu ya mbegu na utaongeza mavuno ya haki. Tukitajirishwa kwa kila njia ili tuweze kuwa na ukarimu kwa kila hali na kwamba ukarimu wetu ukupatie Wewe shukrani (2Kor 9: 10 – 11).

Tunataka kwamba pasipo kukoma kwa ajili ya kanisa tukiomba kwamba utatujaza na maarifa ya mapenzi yako, na pia hekima na ufahamu wa kiroho. Na tunaomba hili ili tupate kuishi maisha yanayokustahili, Bwana, na kwamba tupate kukupendeza katika kila njia, tukizaa matunda kwa kila kazi njema (Kol 1: 2 – 11).

Baba, tunaomba siku zote kwamba utuhesabu kamba tunaustahi wito wako, na kwamba kwa uweza wako tupate kutimiza kila kusudi lako jema, na kwamba kila tunalolifanya, lichochewe na imani. Tunaomba hili ili jina la bwana wetu Yesu litukuzwe (2The 1: 11 – 12). Baba, tunaomba kwamba utuokoe na watu wabaya na waovu. Wewe ni mwaminifu, na utatufanya imara na kutulinda na yule mwovu. Baba, ijaze mioyo yetu na upendo wa Mungu na saburi ya Kristo (2The 3: 1 – 5).

Nitayainua macho yangu niitazame milima – msaada wangu utatoka wapi?

Msaada wangu u katika Bwana aliyezifanya mbingu na nchi. Asiuache mguu wako usogezwe – asisinzie akulindaye. Naam, hatasinzia wala hatalala usingizi, Yeye aliye mlinzi wa Israeli.

Bwana ndiye mlinzi wako – Bwana ni uvuli mkono wako wa kuume.

Jua halitakupiga mchana, wala mwezi wakati wa usiku. Bwana atakulinda na mabaya yote – atakulinda nafsi yako. Bwana takulinda utokapo na uingiapo, tangu sasa na hata milele (Zab 121).